MWASHITA SAVING & CREDIT CO OPERATIVE SOCIETY LTD'

P.O.BOX. 1410, DODOMA.

TEL. 026 – 2322720

Email: mwashitasaccos@yahoo.com

NAMBA YA USAJILI; DOR 535

MASHARTI YA CHAMA

YALIYOANDALIWA CHINI YA SHERIA YA USHIRIKA NO. 6 YA MWAKA 2013 NA KANUNI ZA MWAKA 2015

Yameandaliwa na Bodi ya chama

@2019/2020

NAKALA;

-MRAJISI MSAIDIZI MKOA

-AFISA USHIRIKA JIJI

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 07/05/2026

MWASHITA SAVINGS AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LIMITED

P.O.BOX 1410,DODOMA
TEL 026-2322720
Email;mwashitasaccos@yahoo.com

REG NO. DOR 535

UHINDINI.

DODOMA.

MASHARTI YA CHAMA YALIYOANDALIWA CHINI YA SHERIA YA USHIRIKA NO.6 YA MWAKA 2013 NA KANUNI ZA MWAKA 2015.

Yameandaliwa na Bodi ya Chama.
@2019/2020

NAKALA. MRAJIS MSAIDIZI MKOA.
AFISA USHIRIKA JIJI.

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....
Date: 07/05/2016

SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA
(SHERIA NA. 6 YA MWAKA 2013)
KANUNI ZA MWAKA 2015

MASHARTI YA CHAMA CHA MWASHITA SAVINGS AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LTD.



UTANGULIZI.

Maelezo juu ya vifungu vya sheria na kanuni zake vilivyotoa mwongozo wa uandaaji wa Masharti ya Chama.
Kifungu cha 52(1) Mamlaka ya uandaaji wa masharti ya Chama. Uk...1
Kifungu cha 52(2)Mwongozo wa uandaaji wa masharti ya Chama Uk...1
Kifungu cha 52(3)Madhumuni ya uandaaji wa masharti ya chama. Uk...1
Kifungu cha 52(4) Mamlaka kwa Chama katika uendeshaji wa chama Uk...2
Kifungu cha 54(1) Mamlaka ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika kuidhinisha na kuweka lakiri katika masharti ya chama. Uk...2

SEHEMU YA KWANZA
MAMBO YA AWALI.

Jina la Chama Uk.....2
Anwani Uk.....2
Tarehe ya kuandikishwa Uk.....2
Namba ya usajili Uk.....2
Kuanzishwa kwa Chama Uk.....2
Eneo la Chama nk. Uk.....2

SEHEMU YA PILI.
MADHUMUNI.


Madhumuni ya kuanzishwa kwa Chama. Uk.....2
Kuwawezesha wanachama. Uk.....3

SEHEMU YA TATU.
UANACHAMA.

Sifa za kujiunga. Uk.....3
Taratibu za kujiunga, kupokea wanachama, Hisa na kiingilio. Uk.....3
Sifa za Uongozi. Uk..... 4
Taratibu za Uchaguzi. Uk.....5
Kuacha,kufukuzwa au kusimamishwa uanachama na Mkutano Mkuu. Uk.....6&7
Haki na wajibu wa mwanachama. Uk.....8&9

SEHEMU YA NNE.
HISA

Kifungu cha 59(1) kiwango cha chini cha hisa Uk.....9
Kifungu cha 59(1&2) Hisa za hiari Uk.....9
Kifungu cha 60(1) Hisa za hiari kuwa dhamana. Uk.....9
Kifungu cha 61(1) Mwanachama kuzuiliwa kuchukua hisa Uk.....9
Kifungu cha 61(2) Hisa za hiari Uk...9&10



SEHEMU YA TANO.
AKIBA.

1. Akiba za wanachama. Uk.....10&11&1
2. Amana za wanachama Uk.....1
3. Akaunti ya muda maalumu (fixed deposit). Uk.....12&1
4. Dhima ya Mwanachama. Uk.....1
5. Ukomo wa madeni au mahitaji ya ukwasi Uk.....1

SEHEMU YA SITA
MAPATO YA CHAMA.

1. Mali na Vyanzo vya fedha za Chama. Uk.....14&1
2. Usimamizi wa Mapato na fedha za chama Uk.....1
3. Mtaji wa Chama. Uk.....15&16

SEHEMU YA SABA.
UONGOZI.

1. Usimamizi na Uongozi. Uk.....1
2. Shughuli za Mikutano mikuu ya mwaka Uk.....16-1
3. Taratibu za kuitisha mikutano mikuu mbalimbali ya chama. Uk.....1
4. Mahudhurio katika mikutano Uk.....19-2

MAJUKUMU BAADA YA UCHAGUZI

1. Majukumu ya Bodi. Uk.....20-2
2. Majukumu ya Kamati ya mikopo. Uk.....22-2
3. Majukumu ya kamati ya elimu na mafunzo Uk.....23-2
4. Majukumu ya kamati ya Usimamizi. Uk.....24-2
5. Majukumu ya Meneja. Uk.....25-2

SEHEMU YA NANE.

1. Taratibu za uwekaji na utoaji wa pesa. Uk.....2

SEHEMU YA TISA
UKOPESHAJI.

1. Maana ya sera Uk.....28
2. Sera ya mikopo, aina za mikopo na taratibu za mikopo(rejea ukurasa wa 31-36) Uk.....28
3. Maombi ya mikopo. Uk.....28
4. Uidhinishwaji wa mikopo. Uk.....29
5. Dhamana za mikopo. Uk.....29
6. Udhamini wa mikopo Uk.....29-3
7. Utolewaji wa mikopo na muda wa malipo Uk.....3
8. Uwekaji wa kiwango cha riba, ada na adhabu. Uk.....3
9. Urejeshaji wa mikopo, aina za mikopo na taratibu za mikopo Uk.....30-3

SEHEMU YA KUMI.
MGAO.

1. Mgao wa ziada Uk.....36 -3
2. Matengo ya kisheria Uk.....37-3

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 07/05/2026

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
KUMBUKUMBU.

1. Uhifadhi wa kumbukumbu na tahadhari dhidi ya maafa. Uk.....38
2. Uhasibu Uk.....38-39
3. Ukaguzi Uk.....39

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
UHIFADHI WA AKIBA


1. Uhifadhi wa akiba na fedha nyingine za Chama Uk.....39-40

SEHEMU YA KUMI NA TATU.
MENGINEYO.

1. Utendaji Uk.....40-41
2. Uthibitisho wa wajumbe wa Bodi. Uk.....41

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....
Date: 07/05/2026

SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA
(SHERIA NA. 6 YA MWAKA 2013)



UTANGULIZI.

MASHARTI YA CHAMA CHA MWASHITA SAVINGS AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LTD.

Yametungwa chini ya kifungu cha 52(1), (2), (3) & (4)

Kifungu cha 52.1 "Kila Chama cha Ushirika kitakuwa na mamlaka ya kuanda masharti kwa ajili ya masuala yote muhimu au yanayotakiwa kuendana na dhumuni la kuundwa kwa Chama hicho."
("Every registered society shall have power to make by-laws for any such things as are necessary or desirable for the purpose for which such society is established")

Kifungu cha 52.2 "Bila kuathiri yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1), kwa ujumla wake kila chama cha Ushirika kinaweza kutunga masharti yanayoainisha masuala yafuatayo",
("Without prejudice to the generality of subsection (I), every registered society may make by-laws prescribing";

a) Jina la Chama na anuani ya Chama
b) Eneo la Chama la kuendeshea shughuli zake za kila siku
c) Madhumuni ya kuundwa kwa Chama
d) Azma ya matumizi ya fedha za Chama na jinsi ya kutunza na kuwekeza fedha hizo.
e) Sifa za uanachama, taratibu za kupokea Wanachama, hisa, ada ya kiingilio na utaratibu wa uchaguzi.
f) Dhima ya Wanachama
g) Kuacha, kufukuzwa, kusimamishwa Uanachama na malipo yote yatakayolipwa kwa wanachama hao.
h) Uhamisho wa hisa au faida ya Wanachama
i) Namna ya kuendesha Mikutano ya Chama na mamlaka ya mikutano hiyo.
j) Kuteuliwa,kusimamishwa na kuondolewa kwa Wajumbe wa Bodi na watumishi,na mamlaka na wajibu wa Bodi na watumishi.
k) Kuidhinishwa kwa mtumishi kwa ajili ya kutia saini kwenye nyaraka na kutumia lakiri kwa niaba ya Chama.

Kifungu cha 52.3 Endapo madhumuni ya Chama kilichoandikishwa yanajumuisha kuanzisha mfuko wa wanachama (mtaji wa kukopeshana) yataandaliwa masharti ya ziada yatakayoainisha yafuatayo;
("Where the objects of the registered society includes the creation of funds to be lent to the members additional by- laws shall be made up in respect of;

a) Masharti ya mkopo kwa wanachama ambayo ni;
i. Kiwango cha riba
ii. Muda utakaotolewa kwa ajili ya urejeshaji wa mkopo
iii. Kiasi cha juu cha mkopo utakaotolewa kwa Wanachama
iv. Dhumuni la mkopo anaoomba mwanachama
v. Dhamana za mkopo unaoombwa
vi. Matokeo ya kushindwa kurejesha mkopo katika akaunti ya hisa au amana au mkopo na madhara ya kushindwa kulipa mkopo kulingana na masharti ya mkopo huo.

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....
Date: 07/05/2026

b. Matumizi ya ziada halisi (faida/baki) ya mwaka.
c. Masuala mengine kwa mujibu wa kanuni zinazohusu kampuni ndogo za fedha na ushirika wa fedha.

Kifungu cha 52.4 Masharti yatakayoandaliwa kwa mujibu wa kifungu hiki, yatakipa mamlaka Chama kutoza faini kwa wanachama wake wanaokiuka masharti ya Chama na faini hiyo itahesabika na kulipwa kwa chama hicho kama deni;

Isipokuwa hakuna faini itakayotozwa kutokana na masharti kwa wanachama hadi yafuatayo yatimizwe-

a. Mwanachama anayetarajiwa kutozwa faini ya kukiuka masharti ya Chama (ikiwa ni kutokuhudhuria mikutano mikuu ya mwaka ama kuhudhuria kwa kuchelewa muda ama kutofuata haki na wajibu wake chamani) awe amepewa notisi ya maandishi ya kusudio la kutozwa faini.
b. Mwanachama ameshindwa kutoa maelezo ya utetezi katika muda uliotolewa kwenye notisi.

Kifungu 54.1 Kinampa mamlaka Mrajisi msaidizi wa Vyama vya Ushirika kuidhinisha na kuweka lakiri katika masharti ya Chama chochote ambacho kimefanya marekebisho ya masharti yake endapo tu, marekebisho hayo ameridhika nayo baada ya kuona hayapingani na sheria hii, ambapo nakala iliyoidhinishwa na kuwekwa lakiri itakuwa ni ushahidi kwamba marekebisho hayo yameandikishwa, lakini pia kama marekebisho hayo yatapingana na sheria hatayaidhinisha.

SEHEMU YA KWANZA

✠ JINA

(a) Jina la Chama litakuwa MWASHITA SAVINGS AND CREDIT CO-OPERATIVE SOCIETY LTD. (MWASACCO)

(b) Anwani ya Chama ni S.L.P. 1410, DODOMA.
TEL. 026 – 2322720
FAX: 026 – 2322720
Email; mwashitasaccos@yahoo.com

(c) Tarehe ya kuandikishwa kwa Chama ni 10th January 1997 kwa Namba ya Usajili DOR 535.

(d) Tarehe ya Chama kuanza shughuli zake rasimi ni January 1998 kikiwa na Idadi ya Wanachama waanzilishi 25.

(e) Eneo la shughuli za chama litakuwa Mkoa wa DODOMA

(f) Makao Makuu ya chama yatakuwa DODOMA.

SEHEMU YA PILI.

✠ MADHUMUNI:

Madhumuni ya kuundwa kwa chama hiki ni haya yafuatayo:

(a) Kupokea Hisa, Akiba na Amana kutoka kwa wanachama na kutoa mikopo yenye riba ndogo na masharti nafuu kwa wanachama wake.

(b) Kutoa huduma mbalimbali katika kila kundi bila kujali kabila wala dini kwa kuzingatia sifa zinazohitajika, taratibu za chama pamoja na masharti ya chama.

(c) Kuwashawishi watu wasio wanachama kujiunga na chama hiki.

(d) Kuwezesha shughuli za wanachama pamoja na kuinua hali ya maisha ya wanachama.

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....
Date: 07/25/2022

(e) Kuwawezesha wanachama kutumia na kutunza vizuri fedha zao kwa manufaa katika mambo yafuatayo:-

i. Kuwahimiza wanachama kuongeza Hisa, Amana na Akiba mara kwa mara katika akaunti zao.

ii. Kuhifadhi fedha katika mashirika ya fedha au kununua dhamana za Serikali baada ya kutekeleza madhumuni muhimu ambayo ni kutoa huduma ya Akiba na Mikopo kwa wanachama.

iii. Kuwawezesha wanachama kusafirisha fedha kwenda/kutoka sehemu mbalimbali za nchi kwa gharama nafuu

iv. Kutoa huduma za kibenki kulingana na mahitaji ya wanachama na wateja.

v. Kutoa Elimu kwa wanachama ili kuwawezesha kujenga Akiba na kutumia mikopo wanayopewa kwa busara.

SEHEMU YA TATU

SIFA ZA KUJIUNGA UANACHAMA, TARATIBU ZA KUPOKEA WANACHAMA, HISA, KIINGILIO, SIFA ZA UONGOZI NA TARATIBU ZA UCHAGUZI.

A. SIFA ZA KUJIUNGA UANACHAMA.

(a) Awe Mkazi wa Mkoa wa Dodoma hususani ndani ya Halimashauri ya JIJI la Dodoma (kwa maana ya kuishi karibu na eneo la chama hiki) na awe anafahamika na wanachama wenzake.

(b) Awe ametimiza umri wa miaka kumi na nane (18) na kuendelea mpaka miaka 70 mwisho kwa maana ya kulindwa na Bima ya mikopo endapo atakopa mkopo Chamani.

(c) Awe ni Raia wa Tanzania mwenye akili timamu na asiwe amehukumiwa kesi yoyote mahakamani wala kufungwa Jela.

(d) Awe mwaminifu Chamani mwenye kukilinda na kukisimamia chama kwa haki dhidi ya wizi, ubadhilifu, rushwa, utapeli nk.

B. TARATIBU ZA KUJIUNGA, KUPOKEA WANACHAMA, HISA NA KIINGILIO.

(e) Mtu anayependa kujiunga na chama atatakiwa kununua fomu ya maombi ya uanachama kwa sh 5,000/= tu maombi hayo yatarudishwa pamoja na picha tatu za rangi ya bluu (pasiport size) pamoja na kopi ya kitambulisho cha uraia au mpiga kura, maombi hayo yatapelekwa kwa Meneja na baadae kujadiliwa na Bodi ya Uongozi ambapo Uongozi huo baada ya majadiliano unaweza kukubali au kukataa maombi hayo.

(f) Mwombaji akiridhika Na taratibu zote pamoja Na masharti ya Chama, Na endapo Uongozi utampitisha baada ya kuridhika Na maombi yake, atatakiwa kulipa kiingilio cha tsh 70,000/= kama kilivyoidhinishwa na Mkutano mkuu mwaka 2019 fedha ambayo Sheria Na.6 ya mwaka 2015 kifungu cha 72(1) a

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....
Date: 07/05/2026

kinasema kwamba, kiingilio hakitarudishwa endap
Mwanachama atajifuta uanachama, labda tu pale ambap
maombi ya uanachama yamekataliwa. Na kwa mujibu w
kanuni ya jumla ya Vyama vya Ushirika namba 38(3) y
mwaka 2014.

(g) Mwombaji akishakamilisha malipo ya kiingilio atatakiw
kulipa hisa kumi(10) za kuanzia kiasi cha tsh 300,000/
ambazo ni sh 30,000/= kwa kila hisa moja, lakini atatakiw
kutimiza hisa 15 za tsh 450,000/= na kuendelea baada y
kumaliza mwaka mmoja chamani tangu siku amejiunga a
kama amekopa mara moja na kuhitaji mkopo wa pili, n
baada ya taratibu hizo atatia saini katika daftari la wanacham
kwa maana ya usajili, Hii ni pamoja na wanacham
waliojifuta nyuma kwa sababu zinazoeleweka na baaday
kuamua kujiunga tena na Chama.

(h) Sambamba na hilo Mwanachama ambaye uanachama wak
umekoma au ataamua kujifuta uanachama, atatakiwa kuto
taarifa ya maandishi ya siku 60 yaani miezi miwili ikionyesh
kusudio la kujifuta uanachama, siku 60 zitakapoish
atarudishiwa hisa, akiba na amana zake zote zilizokuwep
chamani"endapo hana mkopo na wala hajadhamini mkop
wowote chamani. Pia Meneja na Bodi hawana maamuzi y
kumfuta uanachama mpaka maamuzi ya Mkutano mku
ukubaliane na ombi hilo.

(i) Uanachama unaweza kuwa wa mtu binafsi au vikund
vinavyofanya kazi zake katika eneo la chama.

(j) Chama kitakuwa na daftari la uanachama lenye maelez
muhimu ya mwanachama ambayo yatathibitishwa kwa sahih
yake.

C. SIFA ZA UONGOZI.

Ikiwa ni sehemu ya haki na wajibu wa mwanachama, sheria Na.6 y
mwaka 2013 kifungu cha 43 kinasema, "kila mwanachama atakuw
na kura moja tu katika shughuli za chama na atakuwa na haki y
kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Chama na kura yake itahesabiw
katika jambo lolote linalohitaji uamuzi katika Mkutano huo.
Sambamba na hilo Uchaguzi wa Viongozi wa Bodi na kamati y
Usimamizi kwa mujibu wa kanuni ya mwaka 2015 kifungu cha 39
(1 -9) na kifungu cha 40(1-5) iliyotungwa chini ya sheria Na 6 y
mwaka 2013 kifungu cha 141(1) na (3) kinasema kwamba
'Mwanachama yeyote anayekusudia kuchaguliwa kuwa mjumbe w
Bodi au Kamati ya usimamizi atapaswa kuzingatia na kufuat
vifungu tajwa hapo juu ikiwa ni pamoja na;

- Sifa zinazositahili kwa mgombea huyo.
- Kujaza fomu za uchaguzi zinazotoa maelezo yake binafsi,
- Uzoefu katika Uongozi na taarifa nyingine zitakazohitajik
kama zilivyoelezwa katika masharti ya SACCOS na Mraji
kwa nyakati tofauti.
- Kuwa mwaminifu na mwadilifu katika uongozi, ukopaji n
urejeshaji wa mikopo ili kuwa na usimamizi mzuri wa Saccos

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.I. Wasonga
Advocate Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 07/05/2026

- Kuwa mwekaji mzuri wa hisa, amana na akiba za kila mwezi.
- Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya 8 mgombea atatakiwa kutangaza mali zake zote, lakini akishindwa atakuwa amekiuka kanuni za maadili na atapoteza sifa yake ya kuchaguliwa kama mjumbe wa Bodi au kamati ya Usimamizi.
- Viongozi hao wanapaswa kuwa na utaalamu au ufahamu wa masuala ya fedha, biashara, Uongozi, au ufahamu na uzoefu wa Uhasibu .(kanuni kifungu Na.(40)3 cha sheria Na. 6 ya mwaka 2013)
- Mjumbe wa Bodi na Kamati ya usimamizi atapaswa kushika wadhifa wake kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuchaguliwa tena ili mradi mjumbe huyo asitumike kwa zaidi ya vipindi viwili mfululizo yaani miaka 6 tu ndio mwisho.(kanuni kifungu Na.(40)4 cha sheria Na. 6 ya mwaka 2013)
- Mtu yeyote hataruhusiwa kushika wadhifa wa kuwa mjumbe wa Bodi au kamati ya usimamizi katika zaidi ya Saccos moja kwa kipindi hicho hicho. (Kanuni kifungu Na (40).5 cha sheria Na 6 ya mwaka 2013).
- Bodi na Kamati ya usimamizi itajumusha wajumbe wanaume na wanawake ambao wamekamilisha kulipa hisa zao. (Kanuni kifungu Na (40).2 cha sheria Na 6 ya mwaka 2013).
- Kila Bodi itakuwa na idadi ya wajumbe katika namba tasa wasiopungua watano na wasiozidi tisa akiwemo Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti. (Kanuni kifungu Na (40).1 cha sheria Na 6 ya mwaka 2013).
- Kwa mujibu wa sheria na.6 ya mwaka 2013 kanuni ya mwaka 2015 kifungu Na.41(1) kinasema, "katika kuendesha shughuli za saccos, wajumbe wa Bodi watapaswa kuzingatia uadilifu na umakini katika kufanya maamuzi yake na watawajibika kwa pamoja kwa hasara yoyote iliyotokana na matendo yao ambayo yamefanywa kinyume na sheria na kanuni hizi.

D. TARATIBU ZA UCHAGUZI.

Kwa mujibu wa sheria Na.6 ya mwaka 2013, uchaguzi wa Bodi na kamati ya usimamizi ni lazima uzingatie yafuatayo;

- Uchaguzi wa Bodi ya Chama utakuwa kwa mujibu wa kanuni ya 42 na 43 ya mwaka 2004 iliyoboreshwa na kuwa kanuni ya mwaka 2015 na kulingana na Kanuni namba 39 ya Vyama vya Ushirika,hatua zifuatazo zitafuatwa wakati wa uchaguzi wa Bodi na kamati ya Usimamizi ambazo ni;
  - (i) Kila uchaguzi utafanyika chini ya usimamizi wa Afisa Ushirika ambaye atakuwa msimamizi wa uchaguzi kama Mrajis atavyoamuru.
  - (ii) Uchaguzi utakuwa kwa kura ya siri kulingana na sheria ya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013
  - (iii) Wale wote watakaohitaji kugombea nafasi mbalimbali chamani, watachukua fomu toka ofisi za chama na watazijaza.

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 07/05/2026

(iv) Fomu zilizojazwa zitapaswa kurudishwa kwa msimamizi wa uchaguzi siku 14 kabla ya siku ya Mkutano wa uchaguzi.

(v) Kamati ya Uchaguzi itapitisha wagombea watakaopigiwa kura wale tu waliofikisha alama 50 au zaidi kati ya alama 100. Kanuni ya mwaka 2015 kifungu cha 39 (6).

(vi) Mkutano Mkuu wa wanachama utakuwa na uamuzi wa mwisho kuhusu orodha ya watakaopigiwa kura.

(vii) Itakapofika agenda ya uchaguzi wa viongozi, Mrajis Msaidizi au Afisa Ushirika wa chama atasimamia uchaguzi wa Mwenyekiti atakayeongoza uchaguzi. Mwenyekiti huyo sharti atoke mingoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu.

(viii) Kutabandikwa tangazo la kuonyesha nafasi za wagombea wa Bodi ya Uongozi na kamati ya usimamizi.

(ix) Wagombea wa nafasi ya ujumbe wa Bodi au kamati ya usimamizi watapewa muda wa dakika tatu kujieleza mbele ya wanachama kabla ya zoezi la kupiga kura kuanza.

(x) Mara tu baada ya uchaguzi kura zitahesabiwa na matokeo kutangazwa na mwenyekiti wa Mkutano.

(xi) Nafasi za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti zitajazwa na wajumbe watakaochaguliwa kwa kupigiwa kura toka kwa wajumbe wa Bodi waliochaguliwa.

(xii) Kama kutakuwa na wagombea zaidi ya wawili kwa nafasi ya Mwenyekiti au Makamu wa Mwenyekiti basi mgombea atakayepata kura nyingi zaidi ndiye atakayetangazwa kuwa mshindi.

(xiii) Wajumbe wa Kamati ya Mikopo na Kamati ya elimu na Uhamasishaji watatokana na wajumbe wa Bodi waliochaguliwa.

(xiv) Wajumbe wa kamati ya Usimamizi watapatikana kwa kuchaguliwa kwa kupigiwa kura ya siri na wanachama katika Mkutano Mkuu.

(xv) Uchaguzi Mkuu wa kawaida, utafanyika kila baada ya miaka mitatu (3) kulingana na Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015 baada ya kujiuzulu 1/3 ya wajumbe wa Bodi na Kamati ya Usimamizi

(xvi) Mambo yafuatayo yatazingatiwa wakati wa Uchaguzi.

- Uchaguzi utafanyika kama agenda mojawapo ya Mkutano Mkuu (siku hiyo hiyo ya Mkutano Mkuu)
- Kila mwanachama atakuwa na kura moja tu.
- Watendaji na maafisa ushirika wataandaa orodha ya wanachama wote ambao wamechelewesha mikopo yao kwani hawataruhusiwa kugombea nafasi yoyote.

E. KUACHA, KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA UANACHAMA NA MKUTANO MKUU.

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....
Date: 07/05/2026

a) Kufukuzwa au kusimamishwa Uanachama na Mkutano mkuu.
Kwa mujibu wa sheria Na 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 53(1) & (2) g Mwanachama anaweza kuachishwa au kusimamishwa uanachama kutokana na mambo yafuatayo;

i. Kushindwa kulipa mkopo katika muda ulioruhusiwa na chama pasipo kuwa na sababu yoyote inayokubalika na Bodi (rejea kanuni ya 2015 kifungu cha 72(1,2,5&6)
ii. Kushindwa kuhudhuria kwenye Mikutano Mikuu ya Chama kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa na sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na chama chenyewe kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, Kanuni kifungu cha 33(1) kinachoamuru Saccos kuitisha Mkutano mkuu,lakini pia kifungu cha 34(1) kinaonyesha shughuli za Mkutano mkuu zinazomlazimu kila mwanachama kuhudhuria kwenye Mkutano.
iii. Kukosa uaminifu kwenye Chama hususani katika matumizi mabaya ya fedha za wanachama mfano kukopa na kukimbia inaonyesha kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu mpaka kupelekea kupelekwa mahakamani.
iv. Kufanya kitendo chochote ambacho Bodi na Mkutano mkuu itaridhika kuwa ni cha kutokuwa mwaminifu au ambacho ni kinyume cha madhumuni ya vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo.
v. Kukiuka Sheria ya vyama vya Ushirika pamoja na kanuni zake zote kwa ujumla juu ya uanzishwaji wa Saccos na hasa katika haki na wajibu wa kila mwanachama mfano uwekaji wa Hisa na akiba
vi. Kuonyesha nia ya kupokea au kutoa rushwa kwa mtendaji wa saccos.

b. Kukoma au kuacha Uanachama:
Mwanachama anaweza kuacha uanachama katika mambo yafuatayo;

(a) Kujiuzulu mwenyewe baada ya kutoa taarifa ya miezi miwili (siku 60) kwa maandishi kwa Bodi ya Uongozi.(kifungu cha (52)(2)
(b) Mwanachama anapofariki dunia.
(c) Mwanachama anapochukua Hisa zake zote chamani
(d) Mwanachama kupata ugonjwa wa kichaa (Wazimu) ulithibitishwa.
(e) Mwanachama akihama katika eneo la Chama hiki kimakazi au kikazi.
(f) Kukataliwa uanachama na theluthi mbili ya wanachama waliohudhuria katika Mkutano Mkuu baada ya kupewa nafasi ya kujitetea baada ya kufanya makosa ambayo yanalazimu kukataliwa uanachama.
(g) Kufilisika kwa Chama

c. Kujiunga upya.
Mtu aliyeacha au kufukuzwa uanachama kwa sababu zinazoeleweka anaweza kujiunga tena kwa mujibu wa masharti haya. Hata hivyo mwanachama aliyewahi kufukuzwa itabidi apate idhini ya Mkutano Mkuu kabla ya kujiunga tena na Chama na endapo mwanachama atajiunga

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 7/05/2026

atamteua mrithi wake ambaye atakuwa na haki ya kulipwa Hisa na faida zozote za chama. Pia Mwanachama huyo atakuwa na haki ya kubadilisha jina la mrithi ambapo uteuzi huo utaandikwa katika daftari la wanachama na mwanachama anayehusika atatia saini.

F. HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA.

Kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 42 - 51 pamoja na kanuni ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2014 kifungu cha 31-33 mwanachama yeyote atakuwa na haki na wajibu kama ifuatavyo:-

A. HAKI ZA MWANACHAMA:

i. Haki ya kushiriki katika shughuli zote za chama, kwa kufuata Sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na taratibu za Chama zilizowekwa.

ii. Haki ya kuhudhuria na kutoa maoni katika Mikutano mikuu ya chama.

iii. Haki ya kuchagua na kuchaguliwa kuwa Kiongozi wa Chama.

iv. Haki ya kudai Cheti cha hisa baada ya kukamilisha malipo yanayostahili.

v. Haki ya kupewa taarifa zozote zinazohusiana na chama

vi. Haki ya kuweka na kutoa amana na akiba kwa kufuata kanuni na taratibu za chama endapo akiba hizo hazijakopea.

vii. Haki ya kupatiwa mkopo kwa ajili ya kuongeza tija na maendeleo ya kijamii

viii. Haki ya kutazama masharti, mizania, mihtasari ya Mikutano Mikuu na nyaraka za Mrajis wakati wa saa za kazi.

ix. Haki ya kuishauri Bodi ya Chama juu ya uboreshaj wa Chama.

x. Haki ya kuongoza na kuongozwa.

B. WAJIBU WA MWANACHAMA:

Kwa mujibu wa sheria Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni za mwaka 2015, wajibu wa Mwanachama kwa Mwashita Saccos ni kama ifuatavyo;

i. Kufuata masharti ya chama, maadili ya chama, shughuli za Chama, miongozo na Sera mbalimbali za chama.

ii. Kulipa viingilio, kununua hisa na kulipa michango yoyote ya chama itakayojitokeza ambayo itakuwa kwenye masharti ya chama.

iii. Kushiriki katika shughuli zote za Chama kama zinavyoelekezwa na sheria ndogo ya chama.

iv. Kushiriki katika mikutano mikuu ya chama bila kukosa ili kuweza kusoma taarifa mbalimbali za chama pamoja na kutoa maoni, ushauri na maazimio. Rejea kanuni ya 2015 kifungu cha 34(1) & (2).

v. Kubeba dhamana ya chama ikiwa janga lolote litatokea.

vi. Kukopa kwa busara na kulipa kwa wakati kwa maana ya kulipa mkopo kwa wakati uliopangwa, rejea kanuni ya 2015 kifungu cha 63 - 70 kilichotungwa chini ya sheria Na.6 ya mwaka 2013 kifungu cha 141(1).

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 07/08/2016

vii. Mdhamini kulipa mkopo alioudhamini endapo mkopaji atashindwa kulipa mkopo wake bila sababu za maana. Sheria Na. 20 ya mwaka 2003 kifungu cha 66(2), sheria iliyofanyiwa marekebisho na kuwa sheria Na.6 ya mwaka 2013.

viii. Kuweka akiba mara kwa mara na hasa akiba za lazima za kila mwezi.

ix. Kulinda na kuhifadhi vizuri mali za chama

x. Kwa mujibu wa sheria Na.6 ya mwaka 2013, kifungu cha 42(3) kinasema, Mtu hataruhusiwa kuwa mwanachama katika vyama zaidi ya kimoja vilivyo na madhumuni yanayolingana isipokuwa pale chama hicho kinapopata idhini kutoka kwa Mrajisi.

SEHEMU YA NNE

HISA ZA CHAMA:

Kwa mujibu wa Sheria Na.6 ya mwaka 2013 kifungu cha 47(3) kinaeleza; *"Kila chama cha Ushirika kitafanya uthamini wa hisa kila baada ya miaka mitatu, uthaminishaji mwingine wa mali na hisa utafanywa na mthaminishaji aliyeidhinishwa."*

Na kwa mujibu wa kanuni ya 2015 kifungu cha 59(1, 2, &3) kanuni iliyotungwa chini ya sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 141(1) kinaeleza kwamba,

- *59(1) Kila SACCOS itaainisha kiwango cha chini cha idadi za Hisa za uanachama kwa thamani halisi iliyooneshwa katika cheti cha hisa ambacho mtu anaweza kununua kuwa mwanachama.*
- *59(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) SACCOS inaweza kukubali wanachama wake kununua hisa za hiari.*
- *59 (3) Hisa za hiari zinaweza kutumika Kama dhamana ya mkopo kutoka kwenye SACCOS, ila mwanachama hataruhusiwa kutumia hisa za uanachama kama dhamana ya mkopo husika.*

Kifungu cha 60(1) cha kanuni ya mwaka 2015 kinaeleza kwamba, *"Isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo na TUME, SACCOS inapaswa kutumia tu hisa za hiari na akiba kama dhamana kwa mkopo."*

Kifungu cha 61(1) a-c cha kanuni ya mwaka 2015 kinaeleza kwamba, *"Mwanachama hatapaswa kuchukua hisa za uanachama isipokuwa;*

A) Mwanachama anapokoma uanachama au kufariki.
B) Taarifa ya mahesabu ya mwisho imekaguliwa hivi karibuni
C) Saccos ina malimbikizo ya faida halisi.

Kifungu cha 61(2) kinasema, *"Hisa za hiari au akiba zinaweza kuchukuliwa wakati wowote, ilimradi hazijatumika kama dhamana ya mkopo wowote wa mwanachama."*

Hivyo, kwa mujibu wa vifungu vya Sheria hapo juu, Chama kimehakikisha kwamba kila mwanachama amenunua hisa, ambapo kwa sasa Hisa moja ya Chama ina thamani ya shilingi 30,000/= na kila Mwanachama atatakiwa kuwa na Hisa 15 yaani Tshs. 450,000/= mpaka itakapoazimiwa tena na wanachama kwa maana ya kufanya uthaminishaji wa hisa, lakini pia kwa mwanachama mpya anayeanza ataanza na hisa kumi yaani tsh 300,000/=

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 07/05/20

na atatakiwa kutimiza hisa 15 yaani tsh 450,000 baada ya kumaliza mwaka mmoja tangu siku amejiunga chamani **au anapokopa mkopo wa mara ya pili hata kama hajamaliza mwaka chamani.**

- Sambamba na hilo, hakuna mwanachama yeyote atakayeruhusiwa kuwa na Hisa *zaidi ya* Moja ya tano (1/5) au 20% ya hisa zote za chama. Rejea Sheria Na. 20 ya mwaka 2003 kifungu cha 80(3), sheria iliyofanyiwa marekebisho na kuwa sheria Na.6 ya mwaka 2013.

Masharti mengine ya hisa ni haya yafuatayo;

- Kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 61(3) cha sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kinasema "Mwanachama anayetaka kuchukua Hisa zake zote chamani, atatakiwa kutoa taarifa ya maandishi ya siku 60 ikionyesha kusudio la kujifuta uanachama."
- Mwanachama aliye na mkopo au amedhamini mkopo hataruhusiwa kujifuta uanachama kwa maana ya kutoa hisa zake mpaka mkopo ule umemalizika.
- Mwanachama atakayekuwa na Hisa chini ya kumi na tano (15) kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo bila kutoa taarifa yoyote ya maandishi chamani, akaunti yake itachukuliwa kuwa imesinzia na iwapo hataongeza kiasi cha Hisa hadi kufikia Hisa 15 kwa muda wa mwaka mmoja baada ya kupewa taarifa (notice) na Bodi ya siku 90 anaweza kuondolewa kwenye chama, na kwa idhini ya Mkutano Mkuu Bodi inaweza kufunga akaunti yake husika na fedha zake kuhamishiwa kwenye akaunti ya mfuko wa matengo ya SACCOS, Hivyo Uongozi wa Chama kabla ya kuchukua hatua hiyo, itawalazimu kwanza kumpa mwanachama huyo taarifa (notice) ya siku TISINI (90) kwa maandishi kwa kutumia anuani yake inayofahamika chamani. Rejea kanuni ya mwaka 2015 kifungu cha 62(1 – 6)
- Chama kitatoa GAWIO kwenye hisa za wanachama kila mwaka wa fedha kama kimetengeneza faida na Gawio hilo litatolewa baada ya kuthibitishwa na Mkaguzi aliyeidhinishwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu mara baada ya kujiridhisha na hesabu ya mizania.Rejea sheria Na.6 ya mwaka 2013 kifungu cha 78(1&2)
- Mwanachama hataweza kuhamisha hisa zake au maslahi yake katika chama isipokuwa kwa miongozo ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.
- Sheria Na. 6 ya mwaka 2013, kifungu cha 64 kinaeleza kwamba, 'kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 63, Hisa au faida ya mwanachama katika mtaji wa Chama hazitakamatwa kwa ajili ya kufidia deni au kuuzwa chini ya amri yoyote au amri ya mahakama kutokana na dhima au deni analodaiwa mwanachama na afisa mpokeaji kwa mujibu wa sheria ya ufilisi na uwezo wa kisheria au kufanya madai juu ya hisa au faida hiyo.

SEHEMU YA TANO

1. AKIBA ZA WANACHAMA.

Kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 inasema, *"Chama cha Ushirika kitapokea mapato kutoka kwa wanachama wake kwa mfumo wa AKIBA, hisa na*

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S... V...onga
Advocate. Notary P... ...Commissioner
for ...
Sign ...
Date: ...

amana za wanachama" na kwa mujibu wa kanuni ya mwaka 2015 kifungu cha 58a kinaeleza kwamba *"kila Saccos itapaswa kuandaa sera ya uhamasishaji wa uwekaji wa akiba ili kukuza mtaji wa chama."*

Hivyo, kwa mujibu wa vifungu vya Sheria hapo juu, Chama kupitia Mkutano mkuu mwaka 2014 uliazimia kila mwanachama kuwa na akiba isiyopungua kiasi cha tsh 500,000/= na kuendelea kwa lengo la kukuza mtaji wa chama, badala ya kuwa na akiba ya tsh 100,000/= kama ilivyokuwa awali, hivyo kwa maazimio hayo, Uongozi unapaswa kuhakikisha kila mwanachama mpya na wazamani(mwanzilishi) ametekeleza, ingawaje kwa wanachama wapya watatakiwa kuanza na tsh 350,000/=(laki tatu na nusu) ila mpaka amalizapo mwaka chamani au anakopa mkopo wa pili atatakiwa kuwa ametimiza akiba tsh 500,000/= na kuendelea.

Masharti mengine ya akiba ni haya yafuatayo;

- Mwanachama atatakiwa kuweka akiba mara kwa mara, au akiba ya lazima ya kila mwezi Tshs. 10,000/= na kuendelea chamani ambayo itatumika kujenga mtaji wa kukopeshana.
- Kila mwanachama atatakiwa kuwa na akiba isiyopungua Tshs. 500,000/= ili aruhusiwe kukopa, mwenye akiba pungufu ya Tshs. 500,000/= hataruhusiwa kukopa mkopo wowote chamani, lakini kwa mwanachama mpya ataruhusiwa kukopa kwa kuanza na akiba ya tsh 350,000/= ambapo pia atatakiwa kutimiza akiba tsh 500,000/= mara tu amalizapo mwaka chamani tangu siku amejiunga, au pia kama atahitaji mkopo mkubwa zaidi.
- Akiba aliyoweka mwanachama itatumika kama dhamana ya kwanza na moja wapo ya kigezo cha kupata mkopo kulingana na akiba iliyopo, ambapo mkopo hutolewa mara tatu ya akiba aliyonayo mwanachama.
- Kwa mujibu wa sheria Na. 20 ya mwaka 2003 kifungu cha 81(6), sheria iliyorekebishwa na kuwa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kinasema, "SACCOS itatakiwa kutoa faida juu ya Akiba ambayo italipwa kwa kiwango kitakachokuwa kimepitishwa na Mkutano Mkuu wa wanachama",(*The savings & credit cooperative society may pay interest on the savings and deposits at the rate of interest to be determined by the general meeting.*) ingawaje kwa sasa chama kinalipa 4% ya akiba iliyopo kwenye akaunti ya mwanachama na hasa kwa wanachama wenye sifa tu, kama hawa wafuatao;
  - Wanaokopa kwa busara na kulipa mikopo kwa wakati bila kupigiwa simu ya kukumbushwa.
  - Wanaoweka akiba za lazima za kila mwezi kiasi cha tsh 10,000/=
  - Wanaohudhuria kwenye Mikutano mikuu ya chama kila mwaka.
  - Wanaokichangia Chama kwa kuweka fedha kwenye amana zao pamoja na akaunti za muda maalumu.
  - Waliotimiza hisa 15 zenye thamani ya tsh 450,000/= na akiba tsh 500,000/= na kuendelea.
  - Wanaofuata miongozo, sera mbalimbali na masharti ya chama na hususani katika maazimo yote ambayo wanachama wanajiwekea.

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....

- Wanaofanya juhudi kubwa ya kuleta wanachama wapya wazuri na waaminifu kwenye chama kila mwaka.
- Wanaowafungulia watoto na vijana wao akaunti chamani.

❖ Akiba haitatumika kufutia mkopo wa mwanachama na badala yake mkopaji atatakiwa kufuata jedwali la malipo ya mkopo wake bila kukosa.

❖ Akiba haitapunguzwa hata kidogo ikiwa mwanachama bado ana mkopo unaoendelea kulipwa kwa kuwa akiba hiyo ni dhamana ya kwanza ya mkopo.

❖ Mwanachama atakayetaka kupunguza au kuchukua akiba zake baada ya kumaliza mkopo au hata kama hana mkopo atatakiwa kuchukua kiwango kinachozidi tsh 500,000/= tu ya akiba alizonazo.

2. AMANA ZA WANACHAMA.

Kwa mujibu wa Sheria Na. 20 ya mwaka 2003 kifungu cha 81(1-6) na kifungu cha 82(a-c), Sheria iliyofanyiwa marekebisho na kuwa sheria Na.6 ya mwaka 2013 kinasema,

- 81(1)"Mwanachama au mteja anaweza kuweka pesa zake na kujulikana kama akiba au amana kwenye akaunti yake ya amana katika SACCOS husika kwa kuangalia kiasi cha fedha ambacho kimeonyeshwa kwenye masharti ya chama."
- 81(2)"Kama amana imeruhusiwa na masharti ya chama, mwanachama au mteja kwa makubaliano na Chama anaweza kuweka fedha zake na kujulikana.kama amana kwa kiasi kilichopitishwa na mkutano".
- 81(3)"Fedha iliyowekwa na mwanachama kwenye SACCOS ni ile iliyokubaliwa na SACCOS"
- 81(4)" Pesa iliyowekwa kwenye akaunti ya Chama, kama amana inaweza kutolewa muda wowote wa saa na siku za kazi kulingana na kiasi kilichokubalika."
- 81(5)" Kiasi cha fedha chochote kitakachozidi kiasi kilichopitishwa katika masharti ya chama kitatakiwa kitolewe taarifa ya siku 30 kwa maandishi ya kuonyesha nia ya kutaka kutoa fedha".
- 81(6)"SACCOS inatakiwa kulipa faida juu ya amana katika kiwango ambacho kitapitishwa na Mkutano mkuu."

Sambamba na hilo, akaunti hii ya amana anaruhusiwa kufungua mwanachama yeyote ili mradi afuate masharti na taratibu za chama, na kiwango cha kufungua akaunti hii kinaanzia tsh 30,000/= na kuendelea.

Masharti mengine ya amana ni haya yafuatayo;

- ✓ Amana inaweza kuwa dhamana ya mkopo wa mwanachama ikisaidiana na akiba kwa makubaliano ya mkataba ya kutokuitoa.
- ✓ Amana inaweza kutumika kama sehemu ya rejesho la mkopo wa mwanachama
- ✓ Amana inaweza kutolewa hata kama mwanachama ana mkopo wake chamani ilimradi tu amana hiyo isiwe imewekwa kama dhamana ya mkopo.
- ✓ Amana inaweza kuwa kama akaunti ya Benk yako kwa maana ya kuweka na kuitoka muda wowote wa saa za kazi.

3. AKAUNTI YA MUDA MAALUM (FIXED DEPOSIT).

Chama cha Ushirika wa Mwashita saccos kwa lengo la kuboresha chama na kuongeza nguvu ya fedha katika kukopeshana, kinawasihi wanachama wote kuwekeza fedha zao kwenye akaunti ya muda maalumu kwa lengo la

kuongeza kasi ya mzunguko wa fedha chamani badala ya kuweka kwenye mabenki, bidhaa hii ya akaunti ya muda maalumu inatoa faida kubwa kwa mwanachama na chama pia.

Hivyo kiwango cha fedha, riba (faida) na muda wa uwekezaji ni kama ifuatavyo;

- Kiwango Cha kuweka fixed deposit (fedha) ni kuanzia tsh 1,000,000/= na kuendelea mpaka hata billion kulingana na uwezo wa mwanachama.
- Muda wa kuwekeza fedha hizo ni kuanzia miezi 3, 6,9,12 mpaka miezi 18.
- Viwango vya riba (rate) au faida ya uwekezaji huo ni kama ifuatavyo;
  1. Miezi mitatu faida tarajiwa ni 3.3%
  2. Miezi sita faida tarajiwa ni 5.5%
  3. Miezi tisa faida tarajiwa ni 8.5%
  4. Miezi kumi na mbili faida tarajiwa ni 11.5%
  5. Miezi kumi na nane faida tarajiwa ni 17.5%

Sambamba na hilo rate (faida) tajwa hapo juu zinaweza kujadiliwa pia na kuweka makubaliano mengine. (Negotiation).

4. DHIMA YA MWANACHAMA

Kwa mujibu wa kifungu Na.46 (2) cha sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kinasema; "Mwanachama wa chama cha ushirika hawezi kuhamisha hisa zake au fidia katika mtaji wa chama au sehemu yake yoyote isipokuwa.

a) Mwanachama huyo amemiliki hisa au faida kwa muda usiopungua miaka mitano.
b) Uhamisho umefanyika kwa Chama au kwa mwanachama wa chama au kwa mtu ambaye maombi yake ya uanachama yamekubaliwa na Bodi; na
c) Mtu huyo amepoteza sifa zilizotajwa katika kifungu cha 21(2) (b-d).

Kifungu Na.46 (3) Hakuna uhamisho wa hisa au fidia utakaokuwa halali na unaoweza kutekelezwa isipokuwa kama,

- Uhamisho huo na jina la anayepokea uhamisho vimeandikishwa kwa kufuata maelekezo ya Bodi ya Chama.
- Uthaminishaji wa hisa umefanyika.

Kifungu Na. 47 (1) Isipokuwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, dhima ya mwanachama kama ipo, itakuwa katika hisa za mwanachama zilizolipiwa na dhima yake itajulikana kama dhima yenye kikomo kwenye hisa.

Sambamba na hilo, Endapo Chama kitafilisika dhima ya mwanachama kwa ajili ya madeni haitazidi kiwango anachodaiwa chamani pamoja na hisa zake.

Kifungu Na 47(2) Endapo katika kanuni za chama itaelezwa wazi kuwa kiasi cha dhima inayotakiwa kulipwa na mwanachama ni kubwa kuliko gharama ya hisa anazomiliki na kiasi hicho kimeeleza bayana kwamba wajibu wa mwanachama na imeelezwa wazi kwamba, dhima itazidi kiasi hicho, dhima hiyo itajulikana kama dhima kwa njia ya udhamini.

5. UKOMO WA MADENI AU MAHITAJI YA UKWASI.

Kwa mujibu wa sheria Na.6 ya mwaka 2013, na kanuni ya mwaka 2015, kanuni kifungu cha 82(1-2) na 83(1-3). Kinaeleza kwamba;

- Kanuni kifungu 82(1) "Wakati wa ukopaji kutoka nje, SACCOS itapaswa kuhakikisha kuwa ukopaji huo hauzidi asilimia ishirini na tano (25%) ya mali zake zote.
- Kanuni kifungu cha 82(2) bila ya kuathiri masharti, kila SACCOS itapaswa kwa nyakati tofauti katika Mkutano mkuu kuweka kiwango cha juu cha mikopo au amana ya mitaji ambayo kinaweza kupokea kutoka kwa watu ambao siyo wanachama wake zikiwemo Benki na Taasisi za fedha na kiwango hicho cha juu kitapaswa kudhinishwa na Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika au TUME.
- Kanuni kifungu Na.83 (1) "SACCOS itapaswa kuchambua mahitaji ya ukwasi kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja kwa hatua za muda mfupi na miezi kumi na mbili kwa hatua za muda mrefu kwa ajili ya kuhakiksha kuwa kuna ukwasi wa kutosha."
- Kanuni kifungu Na.83 (2) "SACCOS itapaswa kuweka mpango wa dharura wa kunusuru hali mbaya ya ukwasi itakayojitokeza."
- Kanuni kifungu Na. 83(3) "SACCOS itapaswa siyo chini ya kipindi cha robo mwaka, kufanya mapitio na kusimamia muundo wa mizania ili kudhibiti majanga ya kiwango cha riba.

Hivyo kutokana na vifungu vya sheria tajwa hapo juu, Chama kwa idhini na maazimio ya Mkutano mkuu kinaweza kukopa kiwango cha juu cha mkopo ambao utakuwa umepitishwa na Wanachama wa mkutano pamoja na kuidhinishwa na Mrajisi msaidizi wa Vyama vya ushirika, na sambamba na hilo chama hakiruhusiwi kukopa nje bila idhini ya makundi tajwa hapo juu.

SEHEMU YA SITA

1. MALI NA VYANZO VYA FEDHA ZA CHAMA:

Kwa mujibu wa sheria Na.6 ya mwaka 2013 kifungu cha 71(1) & 71(2) kinaelezea juu ya mali na upatikanaji wa vyanzo vya mapato ya chama kama ifuatavyo;

Kifungu 71(1) "Mapato ya chama cha ushirika yatakuwa ni pamoja na ;

i. Fedha zote zitakazotokana na Hisa za wanachama pamoja na mauzo ya hisa.
ii. Mapato yote ya chama yatakayotokana na akiba za wanachama za lazima na za hiari pamoja na amana za wanachama.
iii. Fedha zote zitakazotokana na ada au tozo kama itakavyoidhinishwa katika masharti ya chama mfano viingilio vya wanachama wapya, adhabu mbalimbali, michango maalumu, misaada nk.
iv. Fedha zote zitakazotokana na malipo ya michango kama itakavyokubalika mfano michango maalumu ya mfuko wa maendeleo, afya nk.
v. Mapato yote ya chama yatakayotokana na amana na mikopo kutoka kwa watu wasio wanachama kama ilivyoainishwa kwenye masharti ya chama husika.
vi. Fedha zote ambazo chama kinaweza kukopa kutoka taasisi za mikopo mfano mabenki au chanzo kingine chochote ambacho

kwa mamlaka yake chama hicho kinaweza kukusanya fedha kwa njia ya mkopo.

vii. Mauzo ya fomu za mikopo na fomu za uanachama.

viii. Riba juu ya mikopo ya wanachama.

ix. Ziada halisi ya chama.

x. Mapato yatokanayo na miamala mbalimbali ya kifedha kwa njia ya simu.

Kifungu 71(2) "Pato jingine lolote halali ambalo chama kitajiridhisha nalo na ambalo halikuanishwa kwenye mtiririko huu." Mfano akaunti ya muda maalumu.

2. USIMAMIZI WA MAPATO NA FEDHA ZA CHAMA.

Kwa mujibu wa sheria Na.6 ya mwaka 2013 kifungu cha 72(1) (a-d) kinaelezea juu ya kusimamia mapato ya chama kama ifuatavyo;

72(1) Ili kusimamia mapato ya chama, Chama kitahakikisha kuwa;

a) Ada ya kiingilio haitarudishwa isipokuwa pale ambapo maombi ya uanachama yamekataliwa.

b) Amana au mkopo kutoka kwa watu wasio wanachama itazingatia vifungu vya sheria hii pamoja na masharti ya chama.

c) Hisa haitarudishwa isipokuwa kwa mujibu wa kanuni za chama pale ambapo kanuni hizo zinaruhusu ukomboaji huo na kwa namna yoyote kanuni hizo zitaainisha kiwango cha chini cha hisa anazoweka kumiliki wakati akiwa mwanachama.

3. MTAJI WA CHAMA

Kwa mujibu wa kanuni za mwaka 2015 kifungu cha 53(1) & (2) (a-d) kilichotungwa chini ya sheria Na.6 ya mwaka 2013 kifungu cha 141(1) kinaelezea juu ya utoshelezi wa mtaji wa Chama kama ifuatavyo:

Kifungu Na.53 (1) "Ili kufikia kiwango cha chini cha mtaji kinachohitajika, SACCOS/CHAMA kitapaswa kuzingatia yafuatayo;"

a) Mtaji tete usiopungua 8% ya jumla ya mali zote za chama, ambapo angalau 6% ni mtaji msingi wa SACCOS na asilimia isiyozidi 2% itatokana na hisa za uanachama, ambapo,

Mtaji tete (core capital) = Hisa za wanachama+ Malimbikizo ya faida + Matengo. Au (Hisa za wanachama +jumla ya mtaji)

b) Mtaji msingi /mtaji halisi (institutional capital) wa SACCOS usiopungua 6% ya jumla ya mali zote za chama ambapo,

Mtaji msingi/Mtaji halisi (institutional capital) = Hisa + malimbikizo ya faida + matengo - hisa.

b) Viwiainishi vyote tajwa hapo juu vitategemea kanuni za mpito

Kifungu Na.53 (2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) TUME inaweza kupanga viwianishi vya chini vya utoshelevu wa mtaji ambavyo ni vikubwa kwa saccos iwapo saccos,

i.) Ina hasara inayotokana na upungufu wa mtaji.

ii.) Ina uwezekano mkubwa wa kukumbwa na majanga

iii.) Uwepo wa kiwango kikubwa mno cha mali zenye ubora, hafifu nk.

iv.) Chama kukua kwa haraka pasipokuwa na ukuzaji mtaji toshelevu na uthibiti wa majanga.

Vyanzo vingine vya mtaji wa Chama ni;

vi. Akiba na amana za wanachama.

vii. Michango mbalimbali.

viii. Misaada na ruzuku mbalimbali.
ix. Ziada halisi ya mwaka.

Sambamba na hayo kwa mujibu wa vifungu tajwa hapo juu, ili kukuza mtaji wa chama, kila mwanchama wa chama hiki anapaswa kuweka hisa, akiba na amana chamani kulingana na masharti na taratibu za chama na hasa katika kutimiza maazimio tunayojiwekea kila mwaka wa Mkutano mkuu.

- Hivyo basi kila mwanachama atatakiwa kutimiza Hisa 15 yaani tsh 450,000/= na akiba tsh 500,000/= na kuendelea, jambo hili ni lalazima na siyo ombi, lengo la Chama ni kukwepa hasara inayoweza kutokea kutokana na upungufu wa mtaji.

SEHEMU YA SABA

1. USIMAMIZI NA UONGOZI.

Kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 69(1) kinaeleza kwamba, "Usimamizi wa shughuli za Chama upo mikononi mwa Mkutano Mkuu na Bodi ya Uongozi."

- **Na kifungu** 69(2) kinaeleza kwamba, "Maelezo yanayohusu usimamizi wa vyama vya Ushirika yameainishwa katika jedwali la 3 la sheria hii."

Sambamba na hilo Kanuni ya mwaka 2015 kifungu cha 30 na 31 kinaeleza kwamba,

- **Kifungu Na.30** "Mamlaka ya juu ya Saccos yatakuwa kwa Mkutano Mkuu wa wanachama ambao utafanyika angalau mara moja kwa mwaka.
- **Kifungu Na.31** "Kila Mkutano Mkuu wa saccos utachagua Mwenyekiti wa Mkutano huo isipokuwa kwa Mkutano mkuu maalumu ulioitishwa na Mrajisi ilimradi kwamba pasitokee Mwenyekiti wa Mkutano mkuu kuwa Mwenyekiti wa Bodi.

Hivyo basi kila SACCOS itapaswa kuitisha mikutano mikuu ya aina 3 ambayo Ni;

i. **Mkutano Mkuu wa mwaka.**
ii. **Mkutano Mkuu wa kawaida.**
iii. **Mkutano Mkuu Maalumu**

kama inavyoelezwa katika jedwali ta tatu la sheria, lakini pia bila kuathiri matakwa ya sheria na kanuni ndogo (1), **Mkutano mkuu wa mwaka utapaswa, isipokuwa kama imeidhinishwa vinginevyo na TUME, kufanyika ndani ya miezi sita baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha uliopita. Kanuni kifungu cha 33 (1-2).**

2. SHUGHULI ZA MIKUTANO MIKUU YA CHAMA.

i. MKUTANO MKUU WA MWAKA.

Shughuli za Mkutano mkuu wa mwaka kama zilivyoainishwa katika kanuni kifungu Na. 34(1) (a-q) & 34(2) zitakuwa ni hizi zifuatazo;

a) Kuzingatia na kuthibitisha mihitasari ya Mkutano mkuu wa mwaka iliyotangulia na yatokanayo na Mkutano mkuu pamoja na Mkutano mkuu mwingine wowote uliojitokeza ambao haukupitishwa awali.
b) Kupokea na kupitia taarifa za fedha za mwaka, taarifa za **wakaguzi** (COASCO) pamoja na muhutasari wa taarifa ya ukaguzi wa Uongozi au barua ya usimamizi na taarifa nyingine zinazohusika.

c) Kutoa taarifa ya gawio lililotokana na faida iliyopatikana kwa ajili ya kugawanywa.
d) Kupokea, kujadili na kupitisha makisio au Bajeti ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha naofuata.
e) Kupokea, kujadili na kupitisha Mpango mkakati na mipango ya utekelezaji ya SACCOS.
f) Kwa kuzingatia masharti ya sheria, kanuni hizi na masharti ya Chama, kuzingatia na kuamua namna ambavyo ziada halisi yoyote iliyopatikana itakavyogawanywa au kuwekezwa.
g) Kuzingatia na kuridhia marekebisho yoyote katika masharti ya chama.
h) Kupendekeza na kupitisha kiwango cha honoraria kwa ajili ya Bodi, posho za Bodi, ada ya Ukaguzi, au malipo mengine kama ilivyo katika sheria na kanuni hizi.
i) Kuchagua wanachama wa Kamati ya Usimamizi.
j) Kuchagua wajumbe wa Kamati ya Mikopo
k) Kuteua wakaguzi wa nje wa SACCOS mfano Coasco.
l) Kujadili na kupitisha maombi ya Uanachama.
m) Kutoa maamuzi ya rufaa za watu ambao maombi yao ya uanachama yamekataliwa na Bodi.
n) Kuzingatia na kuamua kiwango cha juu ambacho SACCOS inaweza kukopa nje kwa maana ya UKOMO WA MADENI (kanuni kifungu cha 82(1-2) na 83(1-3).)
o) Kusikiliza na kuamua malalamiko yoyote yaliyotolewa na wanachama ambao hawajaridhika na uamuzi wa Bodi, ilimradi notisi ya kusudio la kuleta malalamiko mkutano ilitolewa kwa Meneja angalau siku mbili kabla ya Mkutano mkuu.
p) Kama itaombwa, kusikiliza malalamiko ya mkaguzi yoyote yule ambaye amekataliwa na SACCOS.
q) Kufanya shughuli yoyote ile ya jumla ya SACCOS ambapo taarifa imetolewa kwa wanachama ndani ya muda muafaka.

Kifungu 34(2) kinaeleza kwamba, kwa mujibu wa kifungu cha 52 cha sheria, kila SACCOS itapaswa kuweka katika masharti yake taratibu za kuendesha Mkutano wake mkuu na mikutano maalumu ikiwa ni pamoja na Uchaguzi wa Mwenyekiti na katibu wa mkutano.

ii. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA.

Kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 35(1-2) kilichotungwa chini ya sheria Na.6 ya mwaka 2013 kinaeleza kwamba;
"Kila SACCOS, mbali na mkutano mkuu wa mwaka na mkutano mkuu maalumu, inaweza kuitisha mkutano mkuu wa kawaida kwa lengo la;

i. Kuamua idadi ya wajumbe wa Bodi kwa mujibu wa masharti ya SACCOS pale inapohitajika.
ii. Kurekebisha masharti ya chama ya SACCOS pale inapohitajika
iii. Kujadili kusimamishwa na kufukuzwa kwa mwanachama wa SACCOS pamoja na kupokea wanachama wapya.
iv. Kujadili kuwasimamisha au kuwafukuza wajumbe wa Bodi watakaofanya kazi kinyume na sheria, kanuni na masharti ya Chama.

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 07/05/2026

v. Kuidhinisha upatikanaji (ununuzi) au uuzaji wa mali inayohamishika na isiyohamishika.
vi. Kujadili utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika (tume), sheria, kanuni hizi na masharti ya SACCOS.
vii. Kuidhinisha mikataba na makubaliano ambayo yanatakiwa kuidhinishwa na Mkutano mkuu kwa mujibu wa sheria, kanuni na masharti ya SACCOS.

Kifungu Na.35 (2) kinaeleza kwamba, Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), shughuli za Mkutano mkuu wa kawaida zinaweza kujumuishwa na kujadiliwa kwa pamoja na shughuli za mkutano mkuu wa mwaka uliofafanuliwa chini ya kanuni hizi.

iii. MKUTANO MKUU MAALUMU

Kwa mujibu wa kifungu cha 36(1-3) kilichotungwa chini ya sheria Na.6 ya mwaka 2013 kinaeleza kwamba;

- Kifungu cha 36(1) '"Kwa kuzingatia matakwa ya Jedwali la 3 la sheria, hakuna mkutano mkuu maalumu utakaofanyika isipokuwa kama mkutano huo umeitishwa na angalau moja ya tatu ya (1/3) ya Wanachama au Bodi au Mrajisi."
- Kifungu cha 36(2) "Isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo katika masharti ya CHAMA, endapo mkutano mkuu maalumu umeitishwa na angalau moja ya tatu ya wanachama au Bodi, basi Mkutano huo utakuwa na ajenda moja tu maalumu.
- Kifungu cha 36(3)" Mrajisi au mtu yeyote aliyepewa mamlaka na Mrajisi, anaweza kuitisha na kuongoza Mkutano mkuu maalumu wa CHAMA katika namna na wakati na mahali kama atakavyoelekeza na ataelekeza masuala au ajenda zitakazojadiliwa katika mkutano huo mkuu malumu ilimradi kwamba,

a) Mkutano mkuu maalumu huo utakuwa na mamlaka na utazingatia kanuni husika kwa mujibu wa masharti ya CHAMA na
b) Isipokuwa kama imeamuliwa vinginevyo, gharama za mkutano mkuu maalumu wowote zitakuwa za CHAMA.

- Shughuli nyingine za mikutano mikuu ya mwaka, kawaida na maalumu ni hizi zifuatazo;
  i. Kuthibitisha kuwa idadi ipasayo ya mahudhurio imetimia kabla ya kuanza mkutano.
  ii. Kuweka kiwango cha riba juu ya mikopo na faida juu ya Akiba na amana.
  iii. Kuweka idadi ya Hisa na thamani ya Hisa moja.
  iv. Kuzungumzia mambo mengine yanayohusu maendeleo ya chama kwa ujumla na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa Bodi pamoja na kutoa motisha kwa wafanyakazi.
  v. Kusoma na kupitia taarifa ya Bodi ya utekelezaji ya mwaka mzima hususani katika kufahamu maendeleo ya Chama.
  vi. Kupokea taarifa ya ukaguzi ya Mrajisi na kukubali au kukataa taarifa ya mwaka ya mahesabu ya mizania

vii. Wajumbe wa Bodi hawatalipwa mshahara bali watalipwa posho iliyoidhinishwa na Mkutano Mkuu.(kanuni kifungu cha 43(a-b).

viii. Wanachama kujadili na kuazimia kiwango cha chini na cha juu cha mkopo anaoweza kukopa mwanachama chamani.

ix. Kuchagua wajumbe wa kukiwakilisha chama katika vyama na taasisi nyingine zinazohusika na maendeleo ya chama.

x. Katika kupanga Mikutano Mikuu ya kawaida, itabidi Mkutano mmoja ufanyike angalau miezi miwili kabla ya kufunga hesabu za chama kwa ajili ya kujadili na kupitisha Makisio ya mapato na matumizi, Ukomo wa madeni pamoja na mambo yote yanayohusu maendeleo ya Chama.

xi. Mkutano Mkuu Maalum ulioombwa na wanachama, maombi ni lazima yataje sababu za kutaka Mkutano huo ufanyike na waombaji lazima waweke saini zao na wapeleke maombi hayo kwa Mwenyekiti wa chama cha Ushirika cha Akiba na mikopo na nakala kwa Mrajisi.

3. TARATIBU ZA KUITISHA MIKUTANO MIKUU MBALIMBALI YA CHAMA.

Kwa mujibu wa sheria Na. 20 ya mwaka 2003 kifungu cha 37(1-3) sheria iliyorekebishwa na kuwa sheria Na. 6 ya mwaka 2013, Chama kinatakiwa kuitisha mikutano mikuu kwa kufuata taratibu zifuatazo;

i.) Muda wa matangazo ya Mikutano:-

(a). Mkutano Mkuu wa mwaka taarifa itolewe kwa wanachama ndani ya kipindi cha siku 21 tu, kwamba si chini au zaidi ya siku 21. Kifungu Na.37.(1).

(b). Mkutano Mkuu wa kawaida taarifa itolewe kwa wanachama ndani ya kipindi cha siku 21 tu, kwamba si chini au zaidi ya siku 21. Kifungu Na. 37(1).

(c) Mkutano Mkuu maalumu taarifa itolewe kwa wanachama ndani ya kipindi cha siku 7 tu, kwamba si chini au zaidi ya siku 7, kifungu Na 37(1).

ii.) Matangazo ya mikutano hiyo yabandikwe katika ubao wa matangazo ya ofisi ya chama, taarifa zitumwe kwa njia ya simu na mitandao mbalimbali, pamoja na kutumia taratibu zinazokubalika sehemu hiyo. Kifungu Na.37 (2)

iii.) Matangazo hayo yatabidi yaonyeshe waziwazi tarehe ya Mkutano, saa za mkutano, mahali pa mkutano na mambo yatakayozungumzwa. Kifungu Na.37 (3).

4. MAHUDHURIO KATIKA MIKUTANO.

Kwa mujibu wa sheria Na. 20 ya mwaka 2003 kifungu cha 38(1) sheria iliyorekebishwa na kuwa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 na kanuni ya 47(1-3)

- *Kinaeleza kwamba, "Masharti ya chama yanatakiwa yaonyeshe idadi ya wanachama wa Mkutano mkuu wa chama kwa maana ya kwamba, Mahudhurio katika mikutano ya chama yatabidi kuwa si chini ya wanachama 100 au 50% ya idadi ya wanachama wote ikichukuliwa idadi yoyote iliyo ndogo "*

- *Kifungu Na.38 (2) kinaeleza kwamba "Kwa Mikutano Mikuu ya mwaka na kawaida ikiwa mahudhurio hayatoshi baada ya saa moja zilizopangwa, mkutano utaahirishwa kwa siku saba (7) na baada ya siku saba Mkutano mkuu ulioahirishwa ukiitwa tena na idadi isipotimia basi mkutano huo unaweza kuvunjwa kabisa. Sambamba na hilo Mkutano mkuu maalumu unaweza kuitishwa na Mrajisi kwa idadi yoyote ya wanachama watakaokuwepo na maazimio yote anbayo yangezungumzwa na kuwekwa na wanachama wote basi yatapitishwa na wanachama hao watakaokuwepo na yatatakiwa kufuatwa na wanachama wote kwa kuwa yatakuwa ni maamuzi halali.*

MAJUKUMU YA BODI YA UONGOZI BAADA YA UCHAGUZI.

Kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 2013, kanuni ya mwaka 2015 kifungu cha 42(a-z) baada ya uchaguzi wa wajumbe wa Bodi, Bodi italazimika kufanya yafuatayo;

i. Kuchagua kamati ndogo ya mikopo na kamati ndogo ya elimu
ii. Kufanya mkutano wa kikao cha Bodi kila baada ya miezi mitatu.
iii. Kupokea na kujadili taarifa za maendeleo ya chama kutoka kwenye kamati zake na Menejimenti.
iv. Kufikiria na kupitisha maombi ya mikopo ya wajumbe wa Bodi, kamati ya mikopo, menejimenti ya chama na Kamati ya Usimamizi.
v. Kutumia busara kama wafanya biashara wa kawaida kwamba, Hasara yoyote itakayotokea katika chama kutokana na Bodi kutojali wajibu wao wa madaraka waliyopewa na wanachama, italazimika kufidia hasara hiyo kama itakavyoamuliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Rejea sheria Na.6 ya mwaka 2013.
vi. Kumsimamisha mjumbe wa Bodi kwa kukiuka masharti ya chama ama kwa kushindwa kutimiza wajibu wake wa kazi na hata kupelekea kushindwa kupeleka mapendekezo katika Mkutano Mkuu unaofuata kwa ajili ya kutolewa maamuzi.

Majukumu mengine ya Bodi ni haya yafuatayo;

a) Kuhakikisha Menejimenti inatunza ipasavyo na kwa usahihi kumbukumbu ambazo zitaonesha ukweli ya hali ya kifedha ya SACCOS na kwamba kuna udhibiti wa ndani pamoja na mfumo wa uandaaji, utunzaji na utoaji wa taarifa ulio thabiti.
b) Kuhakikisha kuwa shughuli za SACCOS zinazingatia ipasavyo matakwa ya sheria, kanuni, nyaraka za Mrajis, kanuni za maadili na Masharti ya Chama.
c) Kuhakikisha kwamba hesabu za CHAMA zimeandaliwa na kukaguliwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria, kanuni na masharti ya chama.
d) Kuandaa sera stahiki za rasilimali watu, ukusanyaji wa mikopo, uwekezaji, akiba, fedha, ukwasi au usimamizi wa mali na dhima, utunzaji wa taarifa na sera nyingine kama zitakavyobuniwa na Bodi.
e) Kupanga viwango vya riba kwa ajili ya mikopo, akiba na amana kwa kuzingatia uchambuzi wa kitaalamu wa Meneja uliotumika katika kutathimini uwezo wa saccos kulipa riba husika pamoja na

viwango vya riba vilivyopo katika soko kwa bidhaa zinazofanana na hizo.

f) Kupendekeza malipo ya gawio kwa mkutano mkuu wa mwaka na baadae kwa idhini ya mrajis kwa kuzingatia kanuni ya utoshelevu wa mtaji, gharama, matengo na mahitaji ya kisheria kufikiwa.

g) Baada ya kukasimiwa na mkutano mkuu wa mwaka, kuteua kamati ya mikopo kutoka miongoni mwa wajumbe waliochaguliwa, wajumbe wengine watatakiwa kuwa wenye ufahamu na uzoefu katika masuala ya mikopo na fedha inayowahusu wanachama.

h) Kuweka kwa kusaidiwa na Menejimenti, mipango ya uendelezaji wa saccos na uthibiti wa majanga na kuhakikisha mipango hiyo inapimwa mara kwa mara.

i) Kukutana kwa muda utakaopangwa na katika hali yoyote si chini ya mara moja katika kila robo tatu ya mwaka kwa lengo la kujadili na kupokea taarifa inayohusu hali ya chama na kutoa mwongozo na maelekezo ya kisera kwa menejimenti ya chama.

j) Kuhakikisha Chama kinaweka matengo ya kutosha kwa ajili ya hasara zinazojulikana na zinazoweza kutokea kama inavyohitajika kwa mujibu wa kanuni hizi.

k) Kuhakikisha kwamba mkaguzi wa nje anawasilisha taarifa za fedha na za ukaguzi kwenye mkutano mkuu wa mwaka.

l) Kupitia na kuidhinisha makisio ya mwaka ambayo yatajumuisha mapato na matumizi, mizania na mpango mkakati au mpango wowote.

m) Kuidhinisha taarifa za fedha.

n) Kuwezesha ukaguzi wa vitabu vya hesabu na mtu yeyote aliyeidhinishwa kukagua.

o) Kuwekeza kwa kutumia fedha za ziada katika taasisi mbalimbali kwa kuzingatia sheria, kanuni, masharti ya chama, na sera ya uwekezaji ya Chama.

p) Kupendekeza kukopa mikopo kutoka nje mara baada ya kuomba kibali toka wanachama na baadae kupeleka kwa mrajisi kwa ajili ya kuidhinishwa.

q) Kuweka bima ya kutosha pale inapolazimu na kupatikana kwa ajili ya kulinda mali za chama.

r) Kuhakikisha masharti au mkataba unaowafunga wanachama kuhusiana na chama vinazingatiwa.

s) Kufanya upekuzi kwa watu wanaoomba nafasi ya kuwa Meneja wa chama, kuwaajiri na kuweka utaratibu wa ajira yake katika mikataba.

t) Kuwasilishwa taarifa kwa Mrajisi ndani ya siku 14 kuhusu uamuzi wa SACCOS kuajiri, kujiuzuru au kufukuzwa kwa meneja.

u) Kumsimamisha mjumbe yeyote wa Bodi ambaye anakiuka matakwa ya sheria, kanuni na masharti ya chama kwa kusubiri maamuzi ya Mkutano mkuu wa mwaka.

v) Kumsimamisha meneja wa chama, kumpa makalipio ya kinidhamu iwapo utendaji wake hauridhishi na kusitisha mkataba wake wa

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....
Date: 07/05/2026

ajira kwa sababu mbalimbali ikiwemo kutofanya malinganisho kwa taarifa za hesabu katika kipindi cha miezi miwili mfululizo.

w) Kusimamia ufunguaji na uendeshaji wa akaunti za Chama.

x) Kuwapokea wanachama wapya kwa ajili ya kuidhinishwa na mkutano mkuu wa mwaka na kuhakikisha kwamba rejista ya wanachama inatuzwa kwa usahihi.

y) Kutunza rejista ya mahudhurio ya wajumbe wote wa Bodi ambao wanahudhuria vikao vya Bodi.

z) Kuacha kujihusisha na shughuli za kila siku zinazofanywa na meneja na waajiriwa wa SACCOS, hivyo kuwafanya kuwa huru katika utekelezaji wa majukukumu yao na kuwajibika kwa matendo yao.

aa) Kuhudhuria vikao vya Bodi kama vilivyopangwa, na mjumbe wa Bodi atakoma kushika wadhifa wake iwapo atashindwa kuhudhuria vikao viwili mfululizo kwa Bodi inayokutana kila robo mwaka na vikao vitatu mfululizo kwa bodi inayokutana kila mwezi bila ruhusa au sababu ya msingi.

bb) Kuhakikisha kwamba chama kinaendeleza taswira chanya katika tasinia husika na jamii.

SHUGHULI ZA KAMATI YA MIKOPO, ELIMU NA KAMATI YA USIMAMIZI BAADA YA UCHAGUZI. (Chini ya sheria na.6 ya mwaka 2013.)

1. SHUGHULI ZA KAMATI YA MIKOPO.

Kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 50(1) kilichotungwa chini ya sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kinaeleza majukumu ya Kamati ya mikopo kama ifuatavyo;

i) Kamati ya mikopo itapaswa kuwa na wajumbe watatu tu ambao watachaguliwa miongoni mwa wajumbe wa bodi ambapo kwa utatu huo watapaswa kumchagua Mwenyekiti na katibu wa Kamati.

ii) Kukutana mara kwa mara kuzingatia ukubwa wa shughuli zake kwa ajili ya kupitia na kutoa maamuzi, ila isipungue kikao kimoja kwa kila roba mwaka na maamuzi yatafanywa kwa wingi za kura za wajumbe wa kamati na yatawekwa kama kumbukumbu ya kikao.

iii) Kutoa ushauri kwa wanachama kuhusu ukopaji na matumizi ya mikopo yenye busara.

iv) Kufanya mapitio ya maombi ya mikopo na kuyatolea maamuzi kwa kuzingatia kikomo cha mamlaka ya kamati na sera ya mikopo.

v) Kuhakikisha kwamba dhamana ya kutosha yenye majina ya mkopaji imewekwa kwa kila mkopo na kwamba saccos inakuwa na udhibiti wa dhamana husika hadi mkopo wote utakaporejeshwa.

vi) Kufanyia kazi maombi ya mwanachama kuhusu marekebisho kwenye vigezo na masharti ya mkopo ili mradi tu marekebisho hayo yaendane na sera ya mikopo ya chama.

vii) Kuhakikisha kuwa mikopo inatumika kwa makusudi yaliyokusudiwa.

viii) Kutoa kipaumbele kwa maombi ya mikopo yenye kiwango kidogo ekama mahitaji na masharti ya mikopo yako sawa, iwapo fedha zilizopo hazitoshelezi kukidhi maombi yote yaliyoidhinishwaa.

ix) Kwenda kukagua mradi na dhamana za mkopo anaoomba mwanachama kuanzia tsh 5,000,000/= mpaka 50,000,000/=

x) Kutoa ushauri kwa wakopaji kuhusu aina ya mradi anaoombea mkopo pamoja na kuona vyanzo vya mapato ya miradi huo.

xi) Kamati ya mikopo inaweza kuweka kiwango maalum cha mkopo wa dharura ambayo itaidhinishwa na Meneja au Mwenyekiti au katibu wa kamati na baadae kupeleka taarifa kwenye kamati ya mikopo.

xii) Kamati ya mikopo ikisaidiana na maafisa mikopo watachunguza kwa uangalifu sifa za mwombaji mkopo ambazo ni; Mtaji alionao, dhamana za mkopo alizonazo, uwezo wa kulipa mkopo, Hali ya biashara yake au mradi wake, umri au afya yake katika kulipa, historia ya mkopaji katika urejeshaji, tabia ya mkopaji, hali yake kifedha, mtaji unaozunguka kibiashara, vyanzo vya mapato, utunzaji wa kumbukumbu za biashara yake na mengineyo yatakayohitajika na kamati.

xiii) Kamati hii itawajibika kufuatilia matumizi bora ya mikopo na kuhakikisha kwamba wakopaji wanatumia fedha kwa miradi au shughuli waliyoombea mikopo hiyo.

xiv) Kamati ya mikopo itapaswa kukutana na kupitisha maombi ya mikopo angalau mara mbili kwa mwezi yaani mwanzo wa mwezi na mwisho wa mwezi, lakini pia itapaswa kuonana na wakopaji wabaya angalau kila baada ya miezi mitatu.

xv) Kamati ya mikopo inaweza kufanya marejeo ya sera ya mikopo kwa kufanya marekebisho na kupendekeza kwenye Bodi kwa ajili ya marekebisho.

xvi) Kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 73(1) Kamati ya mikopo haitaruhusiwa kutoa mkopo kwa mtu yeyote ambaye siyo mwanachama wa chama.

2. SHUGHULI ZA KAMATI YA ELIMU NA MAFUNZO.

Kwa mujibu wa taratibu za chama, ili chama kipate wanachama wapya wenye ufahamu, uelewa wa masuala ya ushirika lakini pia waaminifu wenye kufuata masharti ya chama, Uongozi utatakiwa kuchagua wajumbe watatu wa kamati ya Elimu na mafunzo toka miongoni mwa Bodi, ambapo majukumu yao ni haya yafuatayo;

i. Kuwaelimisha wanachama juu ya Sheria Na.6 ya mwaka 2013, kanuni zake za mwaka 2015, sera mbalimbali za chama mfano sera za mikopo, sera za uhasibu na fedha, sera za uwekaji akiba na amana, sera za uwekezaji, sera za menejimenti ya ukwasi mali na dhima, sera za ukusanyaji mikopo, sera za elimu ya biashara na ujasiriamali, sera nyingine zitakazotolewa na Mrajisi, Mpango mkakati na mpango biashara wa chama pamoja na miongozo mbalimbali itakayotolewa na Mrajisi.

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....
Date: 07/05/2026

ii. Kuhamasisha wanachama wapya kujiunga kwa njia ya semina, vyombo vya habari nk. mtu mmoja mmoja na kuandaa vipeperushi na matangazo ya shughuli za chama.
iii. Kusaidiana na Meneja kuandaa mabadiliko ya sera, kanuni na masharti ya chama endapo kutatokea mabadiliko yoyote ya sheria kama itakavyoelekezwa na Mrajisi.
iv. Kuhakikisha wanachama wanafuata masharti ya chama na hasa katika uwekaji wa Hisa, akiba na amana chamani.
v. Kusimamia maandalizi ya Mikutano Mikuu ya chama pamoja na semina mbalimbali za chama.
vi. Kutoa elimu nyingine za kijamii kama elimu ya Ukimwi, makazi bora n.k.
vii. Kufuatilia na kuandaa mpango wa elimu kwa wanachama, viongozi na watendaji na kusimamia ratiba ya mafunzo hayo.
viii. Kueneza elimu ya akiba na mikopo yenye riba ndogo na masharti nafuu.
ix. Kusimamia uanzishaji wa matawi ya chama sehemu ambazo kuna uwezekano wa kufanya hivyo.
x. Majukumu mengine kama itakavyoagizwa na Bodi.

3. SHUGHULI ZA KAMATI YA USIMAMIZI

Kwa mujibu wa sheria Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015 kifungu cha 47& 48 kinaelezea muundo wa kamati ya usimamizi pamoja na majukumu ya kamati hiyo kama ifuatavyo;

- Kifungu Na47 (1). Kinaeleza kwamba, "kila kamati ya usimamizi ya Saccos itapaswa kuwa na wajumbe watatu akiwemo Mwenyekiti wa kamati hiyo"
- Na47 (2) kifungu kinaeleza kwamba, angalau mjumbe mmoja wa kamati atapaswa kuwa na uzoefu kwenye masuala ya uhasibu au fedha na uelewa kuhusu viwango na kanuni za ukaguzi, uhasibu na usimamizi wa fedha.
- Kamati ya usimamizi itachaguliwa na Mkutano Mkuu ambapo itawajibika moja kwa moja kwenye Mkutano Mkuu na haitakuwa sehemu ya Bodi ya Uongozi.

Majukumu ya Kamati ya usimamizi yaliyotungwa chini ya kifungu Na. (48) (1-2) ni haya yafuatayo;

a) Kufanya mapitio ya mara kwa mara kuhusu usahihi wa kumbukumbu za hesabu.
b) Kutoa taarifa kwenye kila kikao cha kawaida cha Bodi.
c) Kusimamia na Kutoa mapendekezo ya kuboresha sera, taratibu za uendeshaji na udhibiti wa ndani na kufanya ufuatiliaji wa utekeleazaji wake.
d) Kuandaa taarifa ya ukaguzi na usimamizi wa hesabu ya mwaka na kuiwasilisha kwenye mkutano mkuu wa mwaka kama mkaguzi wa nje hataweza kufanya hivyo.
e) Kupendekeza kwa Bodi wakaguzi wa nje watakaofanya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaofuata; na
f) Kutekeleza majukumu mengine kwa mujibu wa sheria, kanuni hizi na masharti yake.

g) Wajumbe wa kamati hii watatengeneza utaratibu wao wa kutekeleza kazi zao na watapaswa kuchagua katibu miongoni mwao kama mwandishi ambaye atatengeneza na atazihifadhi kumbukumbu zote pamoja na hatua zinazochukuliwa na kamati hiyo.
h) Kusimamia fedha na mali zote za chama kwa niaba ya wanachama.
i) Kamati itafuatilia maendeleo ya miradi mikubwa ya mikopo iliyochukuliwa na wanachama na hasa kama hailipwi ipasavyo na kuhakikisha kwamba mikopo hiyo imelipwa yote.
j) Kamati ya usimamizi itafanya kazi zake zote kwa kushirikiana mara kwa mara na Mrajis wa Vyama vya Ushirika au mwakilishi wake hasa pale wakihitaji ushauri wa sharia ya ushirika.
k) Itatoa au itaamuru uchunguzi ufanyike japo mara moja katika miezi mitatu kama kutajitokeza swala la ubadhilifu wa fedha za chama hiki.
l) Kamati itafanya ukaguzi wa vitabu na itatengeneza au itaamuru utengenezaji wa taarifa itakayotolewa kwa Bodi katika maandishi na itakagua au itaamuru ukaguzi wa mwaka ufanyike na taarifa yake itolewe kwa maandishi katika mkutano mkuu wa mwaka ufuatao.
m) Mwenyekiti wa kamati ya usimamizi atakuwa anakaribishwa kwenye kikao kimoja tu cha Bodi ili kufahamu shughuli za chama zinavyoendelea.
n) Na majukumu mengine kama yatakavyoelekezwa na Mrajisi.

SHUGHULI ZA MENEJA.

26. Kufanikiwa au kushindwa kwa chama kutategemeana na aina ya Meneja wake. Chama chenye Bodi ya Uongozi bora na Meneja mwaminifu, hodari na mwenye ujuzi, kina mategemeo zaidi ya kufanikiwa.

Kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 52(1) kinaeleza kwamba" Kila Saccos itaajiri Meneja mwenye taaluma ya uhasibu, fedha, Uongozi au biashara kufanya shughuli za chama za kila siku".

Kwa mujibu wa kanuni za ushirika za mwaka 2015 kifungu cha 52(2) (a-r) kinaelezea majukumu, kazi, wajibu na madaraka ya Meneja kama ifuatavyo:-

(i) Kutekeleza na kuzingatia sheria, kanuni, sera, taratibu, masharti ya chama na kanuni za maadili.
(ii) Kuhakikisha mifumo ya utendaji na utoaji taarifa ipo madhubuti na inawezesha mawasiliano.
(iii) Kuandaa Bajeti ya mwaka na mpango mkakati wa biashara kwa kushauriana na wajumbe wa Bodi.
(iv) Kuhakikisha shabaha na malengo ya chama yanafikiwa.
(v) Kushughulikia masuala yote yanayowahusu watumishi hususani mafunzo na uendelezaji wa rasilimali watu.
(vi) Kuiwakilisha SACCOS katika shughuli na uingiaji wa mikataba akiwa pamoja na walau mjumbe wa Bodi mmoja, anaweza kuwa mwenyekiti, makamu mwenyekiti au mjumbe yeyote.
(vii) Kuhakikisha vitabu vya hesabu vinafungwa kwa wakati, kumbukumbu za uhasibu zinaendana na hali halisi na

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.I. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: ....
Date: 07/05/2020

zimefanyiwa malinganisho na akaunti binafsi kabla ya kuandaa taarifa ya uhasibu ya mwisho.

(viii) Taarifa ya mapato na matumizi, mizania, na taarifa ya mikopo iliyochelewa zimeandaliwa kwa usahihi na wakati.

(ix) Kutoa taarifa za Menejimenti kwenye vikao vya Bodi ambazo zinaeleza hali ya kifedha ya SACCOS ikiainisha mizania, hesabu ya mapato na matumizi, taarifa ya mikopo iliyochelewa, Bajeti ya mwaka na mwenendo wa SACCOS na uwiano wake.

(x) Kuidhinisha matumizi yaliyoko kwenye makisio kwa viwango vilivyowekwa na Bodi na kutia saini kwenye nyaraka zinazoruhusu utoaji fedha za Saccos kwa kuzingatia ukomo ulioainishwa kwenye sera za Saccos.

(xi) Kuisaidia Bodi kupanga viwango stahiki vya riba, ada na gharama nyingine kwa bidhaa na huduma nyingine zitakazotolewa.

(xii) Kuisaidia Bodi katika kubainisha dhamana zinazokubalika na zinazoweza kutumika kudhamini mikopo.

(xiii) Kuhakikisha kuwa kuna ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya mikopo, uchukuaji wa akiba, na gharama za uendeshaji.

(xiv) Kusimamia ufunguaji na ufungwaji wa akaunti.

(xv) Kuajiri au kuwafukuza kazi watumishi, kulipa mishahara, posho na malipo mengine kama yatakavyoidhinishwa na Bodi, kuwatuza na kuwapandisha vyeo watumishi au kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wakosaji.

(xvi) Kutoa taarifa stahiki kwa mamlaka zinazohusika kwa muda muafaka.

(xvii) Kutekeleza mapendekezo yanayotolewa kwenye taarifa za wakaguzi wa ndani na wa nje na taarifa za kiuchunguzi zinazotolewa na mamlaka husika; na

(xviii) Kufanya shughuli na majukumu mengine kadri ya maelekezo ya Bodi.

(xix) Kusimamia shughuli za kila siku za chama pamoja na kuwa katibu wa Bodi kwenye vikao mbalimbali vya Bodi.

(xx) Kuweka kumbukumbu sahihi za hesabu na nyaraka zingine za chama

(xxi) Kutunza rejista sahihi ya wanachama na Hisa zao.

(xxii) Kusimamia shughuli za utawala, utumishi na maendeleo ya wafanyakazi.

(xxiii) Kutoa mapendekezo kwa Bodi ya uongozi kuhusu maboresho, maendeleo au marekebisho kuhusu sera, sheria na Kanuni.

(xxiv) Kuuza hisa na kutoa hati za umiliki wa hisa kwa wanachama.

Kwa mujibu wa kanuni kifungu cah 52(3) kinaeleza kwamba,' katika kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (2), Meneja atawajibika kwa Bodi.

SEHEMU YA NANE.

TARATIBU ZA UWEKAJI NA UTOAJI WA PESA CHAMANI.

Kwa mujibu wa masharti ya Chama kwa maana ya kuweka kumbukumbu sahihi za mwanachama kila mwanachama atapaswa kuzingatia yafuatayo;

(a) Atapaswa kuwa na kitabu (pass - book) chenye utambulisho wa picha na majina yake ambacho atakitumia yeye mwenyewe katika uwekaji na utoaji wa fedha zake chamani zikiwa ni Hisa, Amana, Akiba, adhabu, faida za akiba na amana pamoja na Mikopo kufuatana na program ya kompyuta.

(b) Vitabu hivyo vitakuwa na namba zinazofuatana ambazo zitasimama kama akaunti namba kwa kila mwanachama na namba hizo pia zitaandikwa katika daftari la wanachama wote, pamoja na leja kadi ya kila mwanachama.

(c) Fedha anazoweka na kutoa mwanachama ni lazima zikatiwe stakabadhi inayoonyesha risti ya kuweka au kutoa na kuingizwa katika kitabu chake (pass - book) na kutiwa saini na mweka hazina (cashier) au mtu mwingine aliyeidhinishwa kupokea fedha, kisha kitabu hicho apewe mwanachama mwenyewe akitunze.

(d) Ikiwa kitabu kitapotea mwanachama anayehusika atawajibika kutoa taarifa ya maandishi kwa mweka hazina (cashier) na baadae cashier kutoa taarifa kwa meneja, ambapo Meneja atamwandikia barua ya Utambulisho kwenda POLICE kwa ajili ya kupatiwa LOSS RIPORT toka police ili chama kiweze kuidhinisha kitabu kingine kwa mwanachama huyo ambapo mwenye kitabu atatakiwa alipie ada ya kitabu kipya tsh 3,000/= au kadri itakavyoamuliwa na Mkutano mkuu na hicho kitabu kipya kitaingizwa salio za hesabu zote za mwanachama kama zilivyokuwa kwa tarehe anayopatiwa kitabu kipya.

(e) Kitabu hicho ni lazima kionyeshwe wakati wote wa kuweka fedha au wakati wa kuchukua fedha ikiwa ni pamoja na mikopo, akiba au amana ili mhasibu aweze kuingiza kiasi kilichowekwa au kuchukuliwa.

(f) Ni marufuku kwa mwanachama kumpa mtu mwingine yeyote kitabu chake na kuja nacho ofisini kwa ajili ya kupatiwa huduma ya kifedha hasa kwa maana ya kutoa fedha kwenye akaunti ya mwanachama mwingne.

(g). Kila mwanachama atapaswa kufika na kitabu chake siku ya Mkutano mkuu wa chama kama kitambulisho chake cha uanachama lakini pia kufahamu kama anazo sifa za kuingia kwenye Mkutano au la.

SEHEMU YA TISA.

SERA, MASHARTI YA UKOPESHAJI NA TARATIBU ZA MIKOPO

Kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 na kanuni za mwaka 2015 kifungu cha63 (1) kinaeleza kwamba, "kila Saccos inapaswa kuwa na sera ya mikopo ya kimaandishi itakayoendana na kanuni hizi na sheria nyingine zinazohusika."

MAANA YA SERA.

Ni mwongozo au utaratibu unaotumika katika kusimamia na kuendesha shughuli za ukopeshaji katika chama cha kuweka na kukopa (Mwashita), ambapo miongozo hiyo ni;

i. Sera za mikopo na
ii. Masharti ya ukopeshaji na Taratibu za mikopo

Ambapo zote kwa ujumla zinaelezea lengo la chama kuwa na miongozo hiyo katika chama, maelezo juu ya miongozo hiyo ni kama ifuatavyo;

- SERA ZA MIKOPO.

Kwa mujibu wa kanuni za mwaka 2015 kifungu cha 63-70 kilichotungwa chini ya sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu Na. 141(1) kinaelezea yafuatayo;

- SERA YA MIKOPO YA CHAMA. (KIFUNGU CHA 63(1&2))

63(1&2) Bodi itafanya mapitio na kuboresha sera ya mikopo angalau kila mwaka na sera husika itajumuisha mambo yafuatayo;

i. Taratibu za ukopeshaji na uwekaji wa kumbukumbu zinazohusika
ii. Vigezo vinavyohitajika kwa ajili ya kupata mkopo
iii. Madhumuni ya mikopo na aina ya dhamana za mikopo zinazokubalika.
iv. Ukomo wa utoaji wa mikopo kwa mwanachama mmoja.
v. Vigezo na masharti kama vile aina za mikopo, kiwango cha riba na utaratibu wa marejesho ya mikopo.
vi. Kiwango cha juu cha mkopo kwa kila bidhaa.
vii. Ukomo wa kiasi cha mkopo kulinganisha na thamani ya dhamana.
viii. Namna ya kubaini uwezo wa mkopaji kurejesha mkopo.
ix. Viwango vya ukomo wa uidhinishaji mikopo wa kamati ya kitaalamu na kamati ya mikopo.
x. Masharti ya dhamana
xi. Ufuatiliaji na tathimini ya ubora wa mikopo.
xii. Utaratibu wa ufuatiliaji na urejeshaji wa mikopo iliyocheleweshwa kulipwa.

- MAOMBI YA MIKOPO. (KIFUNGU CHA 64 (I –VIII).

Maombi yote ya mikopo yatapaswa kufanyika katika fomu maalumu iliyotolewa na CHAMA na itaainisha yafuatayo;

i. Dhumuni la mkopo na kiasi cha mkopo anachoomba mwanachama.
ii. Dhamana inayotolewa pale inapohitajika kwa mkopo alioomba.
iii. Taarifa muhimu za mwanachama zinazotakiwa kama vile anwani, namba za simu.
iv. Hali ya ndoa yake (maridhiano ya kukopa) pamoja na Idadi ya wategemezi ili kuleta picha ya kuonyesha uwezo wake kulipa.
v. Sehemu ya makazi anapoishi na sehemu anayofanyia kazi.
vi. Mapato yake ya sasa, matumizi yake, baki ya mapato yake pamoja na mali zake.
vii. Mikopo mingine anayodaiwa mwanachama toka katika taasisi nyingine za fedha.
viii. Taarifa nyingine za mwanachama kama zitakavyohitajika.

❖ UIDHINISHWAJI WA MIKOPO.(KIFUNGU CHA 65(1&2))

65(1) Mtendaji au mjumbe yeyote katika chama hatapaswa kutoa mkopo bila idhini ya kamati ya mikopo isipokuwa kama kamati ya mikopo imewakasimisha mamlaka yake rasmi ya uidhinishaji wa mkopo wa mwanachama.

65(2) Kamati ya mikopo au waliokasimishwa watahitaji sehemu au dhamana kamili zitakazotolewa kwa mikopo yote.

❖ DHAMANA YA MKOPO (KIFUNGU CHA 66 (1-9))

66(1) Kabla ya kutoa mkopo, Kamati ya mikopo itapaswa kuhakikisha kwamba mkopo husika umedhaminiwa kikamilifu na wanachama hai wawili wenye sifa.

66(2) Mwanachama atapaswa kudhamini mkopo wake kwa kutumia akiba aliyokopea, hisa za hiari kama anazo, amana za muda maalum (fixed deposit), au mali zake mfano nyumba, viwanja na magari, ilimradi mkopo huo usizidi 10% ya mtaji tete wa chama.

66(3) Endapo mkopo wa mwanachama hautadhaminiwa kikamilifu na mkopaji kupitia dhamana kifungu 66(2) tajwa hapo juu, kama atapewa mkopo basi mkopo huo hautapaswa kuzidi 5% ya mtaji tete.

66(4) Endapo mkopo unahusisha dhamana, dhamana hiyo itapaswa kuhodhiwa na chama na kuwekwa vizuri katika kumbukumbu na kusajiliwa ili kukipa chama uwezo wa kumiliki dhamana hiyo kisheria kama italazimu.

66(5) Kama chama kitapokea dhamana za nyumba na viwanja kitapaswa kufanya Uthaminishaji wa dhamana bila upendelo wala kuzingatia mahusiano kati ya mthamini na mwanachama, na pia mwanachama hataruhusiwa kuchagua mthaminishaji wa dhamana zake.

66(6) Mali zote za kudumu atakazotumia mwanachama kama dhamana ya mkopo wake zitapaswa kuwepo karibu na eneo la chama na kwa namna yoyote ile isiwe nje ya Jamhuri ya Tanzania.

66(7) Endapo mmiliki wa dhamana siyo mkopaji, basi mkopaji atatakiwa kuwa na kibali cha maandishi cha kisheria cha kumruhusu kutumia mali hiyo kama dhamana ya mkopo wake.

66(8) Mara mwanachama anapokabidhi dhamana yake, chama kitapaswa kutunza kwenye rejista ya dhamana zote za chama pamoja na kujumuisha taarifa zote muhimu za dhamana.

66(9) Wanachama wanapaswa kufahamu kwamba, hisa za uanachama haziwezi kutumika kama dhamana za mikopo wanayoomba.

❖ UDHAMINI WA MKOPO (KIFUNGU CHA 67 (1-3))

67(1) Kila mwanachama wa mwashita anaweza kudhamini mkopo wa mwanachama mwingine, kama mwanachama huyo;

a) Hajadhamini zaidi ya mkopo mmoja wakati huo huo.
b) Atathibitisha kuwa ana mapato ya kutosha kufanya malipo ya mkopo huo endapo hautarejeshwa.

67(2) CHAMA kitapaswa kumfahamisha bayana kila mdhamini wajibu wake wa kisheria kabla ya kusaini makubaliano ambayo yatampa wajibu wa kuwa mdhamini.

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....
Date: 07/05/2024

67(3) Endapo Chama kimelipwa deni lake kutoka kwa mdhamini, basi kitapaswa kutoa hati ya malipo kwa mdhamini huyo ya kukiri kupokea malipo hayo.

- UTOLEWAJI WA MIKOPO NA MUDA WA MALIPO.(KIFUNGU CHA 68 (1-9)

Kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 73(1) kinaeleza kwamba, *"Chama cha ushirika hakitatoa mkopo kwa mtu yeyote ambaye si mwanachama"* na kwa mujibu wa kanuni za mwaka 2015 kifungu cha 68(1-4) kinaeleza kwamba;

68(1) Isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo na TUME chama kitatoa mikopo kwa wanachama wake tu.

68(2) Chama kitatoza ada kufidia gharama zinazoambatana na utolewaji wa mikopo. (Gharama za fomu za mikopo).

68(3) Endapo kama chama hali ya ukwasi iko chini, chama kitapaswa kutoa kipaumbele kwenye mikopo midogo midogo na yenye muda mfupi wa marejesho na hasa mikopo ya dharura.

68(4) Chama hakitaruhusiwa kutoa mkopo kwa mjumbe wa Bodi, afisa na waajiriwa wengine wa chama au watu wenye uhusiano wa karibu isipokuwa kama mkopo huo umeidhinishwa na idadi kubwa ya kura za wajumbe wa Bodi, pia chama hakitaruhusiwa kutoa mkopo kwa mwanachama kwa upendeleo nje ya utaratibu wa masharti ya chama.

- UWEKEJI WA KIWANGO CHA RIBA, ADA NA ADHABU.

Kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 69 kinaeleza kwamba, "isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo na Mkutano mkuu, Bodi inaweza kupanga viwango vya riba, ada na adhabu vinavyohusiana na mkopo ambavyo vitakuwa vikifanyiwa mapitio ya mara kwa mara na bodi ya Chama.

- UREJESHAJI WA MKOPO.

Kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 70 (2) kinaeleza kwamba, Mwanachama anaweza kurejesha sehemu au mkopo wake wote kabla ya muda wa marejesho na akakwepa kupata adhabu.

- MAKUBALIANO YA MKUTANO MKUU WA CHAMA MWAKA 2014 & 2015 JUU YA SERA ZA MIKOPO PAMOJA NA TARATIBU ZA MIKOPO.

a) SERA ZA MIKOPO YA MWASHITA SACCOS.

Kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 na kanuni za mwaka 2015, Mkutano mkuu uliazimia kuwa na sera mbalimbali za mikopo kama ifuatavyo;

i. Aina za mikopo ya mwashita saccos.

Mwashita Saccos imejikita kutoa mikopo ya aina 10 tofauti tofauti, mikopo hiyo ni;

a) Mikopo ya Biashara
b) Mikopo ya Ujenzi
c) Mikopo ya Ununuzi wa samani mfano gari, television nk.
d) Mikopo ya Elimu

e) Mikopo ya Kilimo.
f) Mikopo ya Ufugaji
g) Mikopo ya Dharura
h) Mikopo ya Bodaboda
i) Mikopo ya Viwanja
j) Mikopo ya Vikundi.

a) Mikopo ya biashara.

Ni mikopo inayotolewa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wakubwa, wa kati na wadogo kulingana na biashara zao na hasa kwa biashara zinazoonekana na ambazo zina muda angalau wa miezi sita tangu kuanzishwa kwake, na mikopo hii inaweza kutolewa kwa mtu binafsi, kikundi au kwa taasisi, *ambapo taratibu za kutolewa kwa mikopo hii zimeelezwa katika kipengele b. cha taratibu za mikopo.*

b) Mikopo ya Ujenzi.

Ni mikopo inayotolewa kwa wanachama wanaohitaji kujenga majengo ya aina mbalimbali mfano nyumba za makazi, nyumba za biashara mfano gesti, godauni, viwanda au ukarabati wa nyumba nk. Mwanachama anapohitaji mkopo huu ni lazima aonyeshe kiwanja au nyumba (pagale) anayoombea mkopo na aeleze vyanzo vya mapato vitakavyomsaidia katika urejeshaji wa mkopo huu, *ambapo taratibu za kutolewa kwa mikopo hii zimeelezwa katika kipengele b. cha taratibu za mikopo.*

c.) Mikopo ya Ununuzi wa samani mfano gari, television nk.

Mikopo hii hutolewa kwa mwanachama yeyote anayehitaji kununua samani tajwa hapo juu ilimradi aonyeshe matumizi halali ya samani hiyo lakini pia aonyeshe invoice ya malipo anayotakiwa kulipa ndipo akabidhiwe mali hiyo kama itahitajika na pia aonyeshe vyanzo vya marejesho ya mkopo huo. , *ambapo taratibu za kutolewa kwa mikopo hii zimeelezwa katika kipengele b. cha taratibu za mikopo.*

d. Mikopo ya Elimu

Mikopo hii hutolewa kwa mwanachama yeyote anayehitaji kufanya malipo ya ada za shule ambapo atatakiwa kuonyesha gharama halisi za ada hiyo zilizoambatana na fomu ya shule ya mwanafunzi huyo, sambamba na hilo atapaswa kuonyesha namna atakavyorejesha mkopo huo mfano kama ni kwa njia ya mshahara ni lazima alete salary slip yake au kama ni kwa biashara ni lazima aonyeshe biashara ilipo na iwe kwa majina yake kwa maana ya lesseni ya biashara, *ambapo taratibu za kutolewa kwa mikopo hii zimeelezwa katika kipengele b. cha taratibu za mikopo.*

e. Mikopo ya Kilimo.

Mikopo hii hutolewa kwa wanachama wakulima wakubwa na wadogo wenye mashamba ya mazao mbalimbali ambapo hutolewa kulingana na mahitaji yao, na ili apate mkopo huu ni lazima awe na shamba ama la kwake ama la kukodi alionyeshe, sambamba na hilo mikopo hii hutolewa kwa namna mbili ambazo ni;

i. Mkopaji anaweza kupewa mkopo wote kwa wakati mmoja kulingana na mahitajii yake.

ii. Mkopaji anaweza kupewa kwa awamu nne tofauti tofauti kama ifuatavyo.

- Fedha kwa ajili ya kulima

Certified as True Copy of the Original
Name: S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: .....
Date: 07/05/2026

- Fedha kwa ajili ya kupanda
- Fedha kwa ajili ya palizi
- Fedha kwa ajili ya kuvuna na kusafirisha mazao hayo.

Sambamba na hilo kwa upande wa urejeshaji, mkopaji atapewa muda wa miezi sita kwanza kulipa riba pekeyake (grace period) na baada ya miezi sita kuisha ndipo ataanza kulipa mkopo wake kwa kipindi cha miezi mitatu kwa kuwa mkopo huu muda wa urejeshaji ni miezi tisa. *Taratibu za kutolewa kwa mikopo hii zimeelezwa katika kipengele b. cha taratibu za mikopo.*

f. Mikopo ya Ufugaji

Mikopo hii hutolewa kwa wanachama wafugaji wakubwa na wadogo wenye mifugo ya aina mbalimbali kama kuku nk. ambapo hutolewa kulingana na mahitaji yao, na ili apate mkopo huu ni lazima awe na mifugo hiyo inayoonekena na kufanyiwa tathimini ya marejesho, ambapo muda wa marejesho ya mikopo hiyo ni miezi tisa tu, na muda wa miezi sita atakuwa akilipa riba tu kwa maana ya (grace period) na miezi mitatu atapaswa kulipa mkopo wote. *Taratibu za kutolewa kwa mikopo hii zimeelezwa katika kipengele b. cha taratibu za mikopo.*

g. Mikopo ya Dharura

Ni mikopo inayotolewa chamani mara moja hata kama mwanachama ana mkopo mwingine chamani ilimradi mwanachama huyo awe na sifa toshelezi za urejeshaji wake na rekodi yake chamani, mikopo hii ya dharura ni kama vile mwanachama kapatwa na tatizo la ugonjwa, kufiwa nk.

h.) Mikopo ya Bodaboda

Ni mikopo ambayo inatolewa sawa na mikopo mingine kwa kufuata taratibu zote za hisa na akiba ya kukopea, bodaboda hizo zitawekwa mwashita kama sampo na mwanachama atachagua na baadae atakopeshwa fedha na mwashita kwa ajili ya kununua bodaboda, aina za bodaboda hizo ni TVS,BOXER, FEKON NK. *Taratibu za kutolewa kwa mikopo hii zimeelezwa katika kipengele b. cha taratibu za mikopo*

I.) Mikopo ya Viwanja.

Ni mikopo ambayo hutolewa kwa mwanachama mwenye sifa chamani na hasa katika kuangalia vyanzo vya mapato yake vitakavyomsaidia kurejesha, chama kitalipa fedha za viwanja hivyo ambavyo mwanachama atakuwa amechagua na baadae mwanachama ataingia kwenye mkataba wa malipo ya mkopo na mwashita saccos. *Taratibu za kutolewa kwa mikopo hii zimeelezwa katika kipengele b. cha taratibu za mikopo.*

J.) Mikopo ya Vikundi.

Ni mikopo inayounganisha kundi la watu 5-10 au zaidi na ndani ya kikundi hicho kila mmoja anaweza kuchukua mkopo kama kikundi ila kulingana na mahitaji yake na wote kwa pamoja ni lazima wadhaminiane kama wanakikundi ila sharti wanakikundi hao wote ni lazima wawe wanachama, kwa kuwa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 73(1) hairuhusu chama kutoa mkopo kwa mtu ambaye siyo mwanachama, udhamini huo unakuwepo endapo mmoja katika kundi hajarejesha basi kundi zima watapaswa kurejesha fedha ya mwenzao, Pia kundi hilo litapaswa kuwa na viongozi watatu watakaopitishwa kwa ajili ya kuweka na kutoa pesa kama watia saini za risti. Kikundi hicho ni lazima kiweke hisa na akiba ili kikopesheke, mfano kama ni kundi la watu 5 ili kundi lichangie tsh 550,000/=, kila mwanakikundi atapaswa kuchangia tsh 110,000/= ikiwa

kiingilio tsh 10,000/=, hisa tano za kuanzia tsh 30,000/= na akiba ya kukopea tsh 70,000/= hivyo kuleta jumla ya tsh 110,000= ambapo mkopo utaanzia na tsh 1,000,000= au zaidi kulingana na kundi lenyewe.

Kikundi hicho chini ya Afisa mikopo kitatakiwa kuwa na sheria zao ndogondogo za kujibana kama zifuatazo;

- Kitatakiwa kuchagua viongozi kwa maana ya Mwenyekiti, Mwekahazina, katibu na wasaidizi wao watakaokuwa wakiweka saini kwenye kutoa na kuweka pesa chamani.
- Kitatakiwa kuwa na daftari la makusanayo ya fedha zao za mkopo tuliowapatia la kila siku, wiki na mwezi.
- Kitatakiwa kuwa na muda maalumu wa kukutana na kuwekeana adhabu mbalimbali kwa atakayechelewa.
- Kitatakiwa kuweka adhabu mbalimbali kwa viongozi au mtu yeyote aliyepewa fedha za marejesho kupeleka mwashita ama hakuzipeleka au kazichelewesha mpaka muda ukapita ama kazipeleka mwashita ila ni pungufu ya alizopewa.
- Kitatakiwa kuweka adhabu mbalimbali kwa mwanakikundi ikitokea kapeleka marejesho yake pungufu ama hakupeleka kabisa.
- Kitatakiwa kuweka utaratibu ikitokea mwanakikundi mwenzao kakimbia na fedha za mkopo bila kufanya marejesho.
- Kitatakiwa kuwa makini katika kuchaguana na hasa katika kuangalia uaminifu wa kila mmoja. Nk.

Taratibu za kutolewa kwa mikopo hii zimeelezwa katika kipengele b. cha taratibu za mikopo.

ii. Aina ya dhamana za mikopo.
iii. Muda wa urejeshaji wa mikopo
iv. Kiwango cha riba juu ya mikopo
v. Aina za wanachama wakopeshwaji nk.

Maelezo juu ya sera za mikopo hapo juu (ii-v) zimeainishwa katika taratibu za mikopo ya mwashita.

b) TARATIBU ZA MIKOPO.

Kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 na kanuni za mwaka 2015, Mkutano mkuu uliazimia kuwa na taratibu mbalimbali za mikopo kama ifuatavyo;

i. Mikopo itatolewa kwa wanachama wa chama hiki tu (sheria Na. 6 ya mwaka 2013, kanuni kifungu cha 73(1).)
ii. Maombi yote ya mikopo yataidhinishwa na kamati ya mikopo ambayo ni lazima ihakikishe kuwa taratibu za chama na masharti ya utoaji mikopo yamezingatiwa na mkopaji. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013, kanuni kifungu cha 65(1).)
iii. Fomu maalum ya maombi ya mkopo itajazwa na kila mwombaji na kuiwasilisha kwa Afisa mikopo na baadae kwa Meneja ambaye ataiwasilisha kwenye kamati ya mikopo, ambapo katika fomu hiyo mwombaji atatakiwa kuonyesha kiasi cha mkopo anaouomba pamoja na dhumuni la mkopo huo. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 64(1-VIII)
iv. Kiwango cha riba kitakachotozwa katika mikopo hiyo ni 1.5% kwa mwezi au 18% kwa mwaka au 27% kwa mwaka mmoja na nusu

kwa mikopo yote ambayo ni mikopo ya kibiashara,vikundi, kijamii, ujenzi, kilimo, ufugaji ,viwanja, bodaboda na elimu ila kwa mkopo wa dharura riba hutozwa 2% tu kwa mwezi. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013, kanuni kifungu cha (69.) &63(2) (v.)

v. Muda wa urejeshaji ni mwaka mmoja mpaka mwaka mmoja na nusu kwa mikopo yote tajwa hapo juu isipokuwa kwa mkopo wa dharura wenyewe muda wa urejeshaji ni miezi minne tu, hivyo mwanachama atachagua mwenyewe muda wa kurejesha. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 63(2) (v.) pamoja na sheria Na. 20 ya mwaka 2003 kifungu cha 95, sheria iliyofanyiwa marekebisho na kuwa sheria Na. 6 ya mwaka 2013

vi. Kiwango cha chini kwa anaeanza kukopa ataanza na millioni moja (1,000,000/=) na kiwango cha juu kinachotolewa mwisho ni million hamsini (50,000,000/=) ila kiwango cha millioni hamsini ni kwa mikopo ya biashara, ujenzi, kijamii nk. ambayo itategemeana na vyanzo vya marejesho kwa viwango hivyo, na kwa mikopo ya kilimo na ufugaji kiwango cha juu ni tsh 25,000,000/= tu ambayo pia chama kitaangalia vyanzo vyake vya mapato, Pia kwa mikopo ya dharura kiwango cha juu cha mkopo ni tsh 5000,000/= tu. . (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 63(2) VI.

vii. Mwombaji atatakiwa kuwa amejiunga na chama kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja chamani yaani siku 30 ndipo aruhusiwe kukopa ingawaje sheria ya Ushirika inasema miezi mitatu.

viii. Kiwango cha mkopo kitatolewa mara tatu ya akiba aliyonayo mwanachama na akiba hiyo isiwe chini ya tsh 500,000/= na kuendelea, kiwango hicho ni maazimio ya mkutano mkuu wa mwaka 2014&2015. Lakini pia rejea Sheria Na.20 ya mwaka 2003 kifungu cha 90(1), sheria iliyofanyiwa marekebisho na kuwa sheria Na. 6 ya mwaka 2013.

ix. Maombi ya mkopo yatatolewa kwa fomu maalumu ya chama, fomu itakayohusu mkopo anaoomba mwanachama ambapo fomu hiyo itatozwa ada ya 0.65% (asilimia) kwa mikopo yote chamani isipokuwa kwa mkopo wa dharura tu ambao utatozwa tsh 1,000/= tu. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 69.)

x. Mkopaji atakatiwa BIMA ya mkopo kwa lengo la kulinda mkopo wake endapo atapata majanga ya muda mrefu mfano kupooza mwili lakini kufariki pia. Bima hizo kwa mwaka 0.77% na kwa mwaka mmoja na nusu ni 1.28%

xi. Mkopaji awe tayari kuridhia kwenye kipengele cha ridhio la ndoa katika kuutambua mkopo. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 64(iv).

xii. Mkopaji kama ni mfanya biashara atatakiwa kuwa na lesseni ya biashara na TIN No. yake lakini kama ni mfanyakazi anataka kulipa kwa mshahara atatakiwa kuonyesha salary slip yake,na kwa mikopo mingine watatakiwa kuonyesha vyanzo vyao vya mapato katika kufanya tathimini ya urejeshaji.

kwa mikopo yote ambayo ni mikopo ya kibiashara,vikundi, kijamii, ujenzi, kilimo, ufugaji ,viwanja, bodaboda na elimu ila kwa mkopo wa dharura riba hutozwa 2% tu kwa mwezi. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013, kanuni kifungu cha (69.) &63(2) (v.)

v. Muda wa urejeshaji ni mwaka mmoja mpaka mwaka mmoja na nusu kwa mikopo yote tajwa hapo juu isipokuwa kwa mkopo wa dharura wenyewe muda wa urejeshaji ni miezi minne tu, hivyo mwanachama atachagua mwenyewe muda wa kurejesha. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 63(2) (v.) pamoja na sheria Na. 20 ya mwaka 2003 kifungu cha 95, sheria iliyofanyiwa marekebisho na kuwa sheria Na. 6 ya mwaka 2013

vi. Kiwango cha chini kwa anaeanza kukopa ataanza na millioni moja (1,000,000/=) na kiwango cha juu kinachotolewa mwisho ni million hamsini (50,000,000/=) ila kiwango cha millioni hamsini ni kwa mikopo ya biashara, ujenzi, kijamii nk. ambayo itategemeana na vyanzo vya marejesho kwa viwango hivyo, na kwa mikopo ya kilimo na ufugaji kiwango cha juu ni tsh 25,000,000/= tu ambayo pia chama kitaangalia vyanzo vyake vya mapato, Pia kwa mikopo ya dharura kiwango cha juu cha mkopo ni tsh 5000,000/= tu. . (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 63(2) VI.

vii. Mwombaji atatakiwa kuwa amejiunga na chama kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja chamani yaani siku 30 ndipo aruhusiwe kukopa ingawaje sheria ya Ushirika inasema miezi mitatu.

viii. Kiwango cha mkopo kitatolewa mara tatu ya akiba aliyonayo mwanachama na akiba hiyo isiwe chini ya tsh 500,000/= na kuendelea, kiwango hicho ni maazimio ya mkutano mkuu wa mwaka 2014&2015. Lakini pia rejea Sheria Na.20 ya mwaka 2003 kifungu cha 90(1), sheria iliyofanyiwa marekebisho na kuwa sheria Na. 6 ya mwaka 2013.

ix. Maombi ya mkopo yatatolewa kwa fomu maalumu ya chama, fomu itakayohusu mkopo anaoomba mwanachama ambapo fomu hiyo itatozwa ada ya 0.65% (asilimia) kwa mikopo yote chamani isipokuwa kwa mkopo wa dharura tu ambao utatozwa tsh 1,000/= tu. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 69.)

x. Mkopaji atakatiwa BIMA ya mkopo kwa lengo la kulinda mkopo wake endapo atapata majanga ya muda mrefu mfano kupooza mwili lakini kufariki pia. Bima hizo kwa mwaka 0.77% na kwa mwaka mmoja na nusu ni 1.28%

xi. Mkopaji awe tayari kuridhia kwenye kipengele cha ridhio la ndoa katika kuutambua mkopo. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 64(iv).

xii. Mkopaji kama ni mfanya biashara atatakiwa kuwa na lesseni ya biashara na TIN No. yake lakini kama ni mfanyakazi anataka kulipa kwa mshahara atatakiwa kuonyesha salary slip yake,na kwa mikopo mingine watatakiwa kuonyesha vyanzo vyao vya mapato katika kufanya tathimini ya urejeshaji.

xiii. Kwa mujibu wa Sheria Na.6 ya mwaka 2013, Kanuni Na.66 (1), masharti ya chama na maazimio yanayotolewa na mkutano mkuu, kamati ya Mikopo itafikiria dhamana kwa kila mkopo kama inatosha na masharti yatakayotumika katika ulipaji. Pia dhamana hizo ni lazima zionyeshwe katika fomu ya maombi ya mkopo. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 66(4).)

xiv. Mkopaji atatakiwa kuweka dhamana za mkopo wake zenye thamani inayozidi 50% ya mkopo anaouomba, na dhamana hizo ni kama vile hati za nyumba, hati za viwanja, kadi za magari na pikipiki, vifaa vya nyumbani na ofisini vyenye thamani inayozidi mkopo wake, sambamba na hilo mkopaji huyo atatakiwa kuwa tayari kufilisiwa dhamana zake na kuuzwa endapo ataacha kulipa mkopo wake kwa wakati (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 63(2) vii.)

xv. Ikiwa fedha za kuwakopesha waombaji wa mikopo hazitoshi, na kama sababu za maombi ni karibu sawa, maombi ya mikopo midogo midogo yatafikiriwa kwanza. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 68(3).

xvi. Hakuna mwanachama yeyote atakayeruhusiwa kufuta mkopo wake kwa akiba bali atatakiwa kuulipa kulingana na mkataba aliousaini.

xvii. Hakuna mwanachama yeyote atakayeruhusiwa kupunguza akiba yake akiwa bado ana mkopo chamani kwa kuwa akiba hiyo ni dhamana namba moja ya mkopo wake. Rejea sheria Na.20 ya mwaka 2003 kifungu cha 90(1), sheria iliyofanyiwa marekebisho na kuwa sheria Na. 6 ya mwaka 2013.

xviii. Mkopaji atatozwa adhabu ya 5% ya malimbikizo ya mkopo wake kila mwezi au 10% ya deni lililosalia baada ya mkataba wake kuishia endapo atacheleweshe mkopo wake. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 69.)

xix. Mkopaji atatozwa tsh 10,000/= au zaidi kulingana na maazimio ya mkutano mkuu kila atakapofatiliwa kama gharama za ufuatiliaji ikiwa ni kuokoa gharama za petrol za pikipiki na matengenezo yake endapo atafuatwa au kuitwa kuonana na kamati juu ya ucheleweshaji wa marejesho yake.

xx. Mwanachama atakayekubaliwa kupata mkopo atadhaminiwa na wanachama hai wawili (2) na wadhamini hao watahusika na malipo ya mkopo wanaoudhamini kwa kiasi kile kilichokopwa endapo aliyedhaminiwa atashindwa kulipa na kila mdhamini atataja dhamana na kiwango anachomdhamini mwanachama mwenzake (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 67 (1-3).)

xxi. Mali inayoondosheka au isiyoondosheka, itakayowekwa dhamana na mkopaji itamilikiwa au itakuwa chini ya udhibiti wa chama mpaka hapo mkopo wote utakapokuwa umelipwa, hivyo mkopo ulioidhinishwa hautatolewa mpaka Meneja atakaporidhika kuwa hati zote muhimu zinazohusiana na umilikaji wa mali zilizowekwa dhamana zimepokelewa na chama

au zimesajiliwa ipasavyo. (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kanuni kifungu cha 66 (4.)

xxii. Mkopaji anaweza kujidhamini mwenyewe ikiwa mkopo anaoomba hauzidi mali zake chamani ambazo ni akiba na amana.

xxiii. Mkopaji hataruhusiwa kutoa amana yake chamani kama amana hiyo ameitaja kama dhamana ya mkopo wake.

xxiv. Mkopaji awe tayari kuthibitishwa na Mwanasheria wa chama au mahakama juu ya umiliki wa dhamana za mkopo wake ili kuleta tija katika urejeshaji endapo ataacha kulipa mkopo wake kwa kukusudia au la.

xxv. Mkopaji na mkopeshaji watatakiwa kusimamiwa na mwanasheria wa chama juu ya makubaliano ya ukopeshaji kwa mihuri na sahihi ya pande zote tatu ambazo ni mkopeshaji, mkopaji na mwanasheria wa chama au mahakama.

xxvi. Kwa mujibu wa sheria Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni za 2015 kifungu cha 72(1) kinaeleza kwamba, *Mkopo wowote ambao malipo ya marejesho yake ni pungufu ya malipo yaliyotakiwa kwa mujibu wa masharti ya mkataba, utapaswa kuchukuliwa kuwa umecheleweshwa,* na kifungu cha 72(2) kinaeleza kwamba, *Mkopo utachukuliwa kuwa umecheleweshwa endapo malipo ya marejesho hayatafanyika ndani ya siku thelathini (30) tangu marejesho hayo kutakiwa kurejeshwa bila kujali mkopo uliocheleweshwa ni riba tu au riba na mkopo msingi,* Hivyo kwa vifungu tajwa hapo juu, kila mwanachama atapaswa kurejesha mkopo wake kulingana na mkataba wake kwa wakati.

C. LENGO LA SERA YA MIKOPO

Chama kupitia sheria ya ushirika imeona ni vyema kuwepo na sera ya mikopo kwa sababu zifuatazo;

I. Kuweka mwongozo mzuri utakaolinda fedha za wanachama.

ii. Inamsaida mwanachama kufahamu wajibu, majukumu na haki zake chamani.

iii. Itawasaidia wanachama uelewa juu ya kukopa kwa busara na kulipa kwa wakati.

iv. Itakisaidia chama kutoa mikopo kwa kufuata utaratibu uliowekwa juu ya ukopeshaji.

v. Itakisaidia chama kutokutoa mikopo inayozidi uwezo wao wa kifedha.

vi. Itakisaidia chama kutokuwa na wadaiwa sugu na wenye madeni mabaya.

vii. Itakisaidia chama kuongeza mapato kwa wakati.

viii. Kwa mujibu wa sheria ni lazima sera hiyo iwepo kimaandishi.

Certified ... Regional ... Commissioner ... Date: 07/05/2020

SEHEMU YA KUMI

1. MGAO WA ZIADA.

Kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 78 (1) kinaeleza kwamba, Chama cha Ushirika hakitalipa gawio au bakhshishi au kugawa sehemu yoyote ya fedha zake zilizokusanywa kabla ya ukaguzi wa mizania utakaofanywa na Mkaguzi aliyeidhinishwa na kupitishwa na mkutano mkuu.

Kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 79(1) kinaeleza kwamba, chama chochote cha ushirika ambacho kitapata faida kutoka katika miamala yake kitadumisha mfuko wa akiba.
Kwa mujibu wa kanuni za mwaka 2015 kifungu cha 55, kanuni zilizotungwa chini ya kifungu cha sheria Na141 (1) kinaeleza kwamba, Kifungu na.55. Kwa kuzingatia masharti, CHAMA kinaweza kugawa ziada yoyote iliyobaki baada ya matumizi na gharama zote kuwa zimelipwa na mahitaji ya mtaji kuwa yamefikiwa kama ilivyoelekezwa katika kanuni ya 53 kwa madhumuni yafuatayo;

a) Gawio la hisa kwa njia ya fedha tasilimu au mawekezo katika hisa za wanachama.
b) Kuchangia katika mfuko wa maendeleo au akaunti ya mtaji wa muda mfupi.
c) Kuchangia katika hisani, elimu, matibabu na madhumuni mengine kwa mujibu wa sheria.
d) Kulipa honoraria kwa wajumbe wa Bodi na maafisa wengine wasiolipwa mishahara; na malipo mengineyo kama yatakavyoidhinishwa na Mkutano mkuu wa mwaka, mfano; motisha kwa wafanyakazi, motisha kwa wanachama walipaji wazuri, kuongeza mtaji wa chama nk.

Hivyo kwa maelezo tajwa hapo juu, endapo chama kitatengeneza faida, Bodi ya chama kwa idhini ya Mkutano mkuu na kwa mujibu wa sheria itatoa gawio la 5% kwa kila hisa alizonazo mwanachama na mgao huu utahusisha wanachama wenye sifa na ambao wametimiza hisa kumi yaani tsh (300,000/=) na kuendelea.

2. MATENGO YA KISHERIA.

Kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 56 (1-5) kinaeleza yafuatayo;
56(1) Chama kitapaswa kujenga mfuko wa matengo na mtaji msingi wake (institutional capital) kwa kubakiza angalau 20% ya mapato halisi baada ya matumizi na gharama zote kulipwa ilimradi kiwiainishi cha mtaji msingi kisiwe chini ya 6% ya jumla ya mali zote za chama.
56(2) Chama hakitapaswa kulipa gawio kwa wanachama isipokuwa pale tu viwianishi vya mtaji msingi (institutional capital) na mtaji msingi halisi kwa mali zote za chama upo na vinalingana na kiwango cha chini kilichowekwa.
56(3) Malipo ya gawio kwa wanachama hayatapaswa kufanyika endapo kiwango kilichopo kwenye mfuko wa matengo ya kisheria hakitoshelezi kufidia malimbikizo ya hasara yaliyofanywa na SACCOS na ziada halisi itahamishiwa kwenye mfuko wa matengo hadi pale bakaa hiyo itakapotosha kufidia hasara husika.
56(4) Bila kujali kanuni ndogo ya (2) na (3), Mrajis anaweza kuidhinisha malipo ya gawio kwa wanachama.
56(5) Isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo na Mrajisi, CHAMA hakitapaswa kutumia akaunti ya mtaji msingi au mtaji tete kama dhamana ya mkopo wa nje.
Na kwa mujibu wa Sheria Na.20 ya mwaka 2003 kifungu cha 67 sheria iliyorekebishwa na kuwa sheria Na.6 ya mwaka 2013 inaeleza juu ya utengaji wa mafungu kama ifuatavyo;

1. AKIBA YA LAZIMA YA KUKOMBOLEA MAFUNGU ni 20%.

Kila mwaka chama kitatenga kiasi kisichopungua (20%) kutokana na faida halisi iliyopatikana kwa mwaka husika kwa ajili ya akiba ya lazima ya kukombolea mafungu na akiba hiyo itabaki kuwa ni mali ya Chama hiki.

2. TENGO LA MIKOPO MIBAYA ni 15%.

Kila mwaka chama kitatenga kiasi kisichopungua (15%) kutokana na faida halisi iliyopatikana kwa mwaka husika kwa ajili ya kinga ya madeni mabaya, lakini kiasi hicho kisizidi asilimia kumi na tano (15%) ya madeni yote.

3. AKIBA YA KUKOMBOLEA HISA Ni 15%.

Kila mwaka chama kitatenga kiasi kisichopungua (15%) kutokana na faida halisi iliyopatikana kwa mwaka husika kwa ajili ya akiba ya kukombolea hisa za wanachama walioacha uanachama au waliofukuzwa uanachama, lakini kiasi hicho kisizidi asilimia kumi na tano (15%) ya mtaji tete na mtaji halisi wa chama. (core capital & institutional capital).

Sambamba na matengo hayo Bodi kwa idhini ya Mkutano mkuu inaweza kutekeleza yafuatayo;

i. Bodi inaweza mara kwa mara kupendekeza katika mkutano mkuu kuongeza mifuko mingine kwa ajili ya maendeleo ya baadaye ya chama, iwapo chama kina mapato halisi ya kutosha.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA.

UHIFADHI WA KUMBUKUMBU NA TAHADHARI DHIDI YA MAAFA, UHASIBU NA UKAGUZI.

Kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 92(1) (a-d) kinaeleza kwamba, CHAMA kitapaswa kila siku kunakili taarifa zote muhimu kwa kutumia kifaa cha kutunza kumbukumbu katika eneo salama lisiloweza kushika moto ambacho ni kasiki, kumbukumbu hizo ni kama vile;

i. Taarifa za uanachama, hisa, akiba,amana na mikopo ya wanachama
ii. Bakaa za mikopo kwa kila akaunti ya mwanachama, uwekezaji wa bakaa katika bank.
iii. Maingizo ya miamala yote kwa kila akaunti kwenye mizania ya mapato na matumizi
iv. Taarifa inayoonyesha orodha ya akaunti za mali, dhima na mtaji kwenye mizania.
v. Sera mbalimbali za chama, SERA ya TUME, sheria na kanuni zake pamoja na masharti ya chama.
vi. Hati za mali za vifaa vinavyomilikiwa na Chama.
vii. Dhamana zilizowekwa na wakopaji
viii. Makubaliano ya mikopo ya nje na sera za chama.

Kwa maelezo hapo juu, chama kinatumia kasiki katika kuhifadhi kumbukumbu mbalimbali za chama.

❖ UHASIBU

Kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 94 (2) & 95 (1-3) kinaelezea shughuli za kihasibu kama ifuatavyo.

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 07/05/2026

i. Kanuni kifungu cha 94 (2) Chama kitapaswa kutoa taarifa kwa mujibu wa viwango vya utoaji wa taarifa za fedha vya kimataifa pamoja na kutunza vitabu vya hesabu na kumbukumbu zingine.
ii. Kanuni kifungu cha 94 (3) kwa ajili ya ufungaji wa hesabu, ukaguzi na utoaji wa taarifa, mwaka wa fedha wa chama hiki utakuwa kuanzia tarehe 1 January hadi kuishia tarehe 31 Desember kwa kila mwaka.
iii. Hesabu za mwisho lazima ziwasilishwe kwa mkaguzi si zaidi ya miezi mitatu baada ya kufunga kwa mwaka.
iv. Kanuni kifungu cha 95(1) Chama kupitia mhasibu kitapaswa kutoa taarifa za fedha angalau kila robo mwaka wa fedha.
v. Kanuni kifungu cha 95(2) Mhasibu atapaswa kubandka taarifa za hesabu za mwaka na taarifa ya ukaguzi wa nje katika ofisi yake kuu kwa ajili ya kupitiwa na wanachama wake.
vi. Mhasibu atapaswa kurejea kifungu cha 92(1) katika kuhakikisha taarifa zote zinatunzwa kwa kumbukumbuku sahihi.
vii. Kupeleka fedha za makusanyo benki siku hiyo hiyo ya makusanyo hayo na kubaki na kiwango kilichopitishwa cha fedha kubaki kwenye kasiki.(sera ya uhasibu na fedha).

❖ UKAGUZI.

Kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 96(1-2) kinaeleza kwamba;

- 96(1) Chama kitapaswa kuwa na ukaguzi wa ndani kulingana na ukubwa wa Chama na hatari inayoweza kujitokeza.
- 96(2) Ukaguzi wa ndani utafanywa na mtu huru mwenye weledi ama ameajiriwa na saccos au ni kamati ya usimamizi.

Kwa maelezo hapo juu, Chama chetu kinakaguliwa na kamati ya Usimamizi ambao majukumu yao yameainishwa katika kanuni za mwaka 2015 kifungu cha 47&.48.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
UHIFADHI WA AKIBA NA FEDHA NYINGINE ZA CHAMA.

Kwa mujibu wa kanuni za mwaka 2015, kifungu cha 81(1&2) kinaeleza kwamba,

Kifungu cha 81(1) "Chama kitapaswa kuhifadhi asilimia 15% ya fedha katika hisa za hiari kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya ukwasi ya haraka.

Kifungu cha 81(2) 'Chama kinaweza kuhifadhi fedha tasilimu kwa ajili ya mahitaji ya fedha kichele tu isipokuwa kiasi cha fedha taslimu kisizidi kiasi kilichoainishwa kwenye masharti.

Katika sheria Na.6 ya mwaka 2013 kifungu cha 75(1) (a-d) na 75(2) vinaeleza kwamba.

- 75(1) Chama kinaweza kuwekeza fedha zake katika mambo yafuatayo;
  - I. Katika amana iliyo na riba kwenye taasisi ya fedha ya ushirika au taasisi yoyote ya fedha kama itakavyoainishwa na Tume.
  - II. Katika hisa za chama chochote cha Ushirika.
  - III. Katika amana za Serikali na dhamana nyinginezo
  - IV. Katika vitega uchumi vinavyoruhusiwa kwa amri ya Mrajisi chini ya usimamizi wa TUME.

Sambamba na vifungu hapo juu, fedha za chama pia zitahifadhiwa

(a) Katika mabenki na kununua Hisa kwenye Makampuni yanayofanya vizuri kwa idhini ya mrajisi.

(b) Kwenye akaunti za muda maalumu katika mabenk tofauti tofauti na hasa benk zenye riba nzuri.

(c) Katika chombo chochote chenye mamlaka ya kuhifadhi akiba ya fedha au dhamana ya umma, na ambacho kitaonekana kinatoa faida zaidi ya mabenki bila kuhatarisha usalama wa fedha za chama.

(d) Kwenye mikopo ya wanachama lakini isizidi (25%) ya jumla ya mali za chama hiki.

SEHEMU YA KUMI NA TATU

MENGINEYO:

UTENDAJI

1. Hakuna mjumbe yeyote wa Bodi wa chama hiki, au mfanyakazi wa Chama hiki atakayeruhusiwa kujiidhinishia au kujiamulia yeye mwenyewe kujilipa fedha za Chama zinazohusu yeye binafsi au Shirika au Kampuni au Chama kingine ambacho anahusika kwa namna yeyote.

2. Wajumbe wa Bodi wote na watumishi wa chama hiki, watatakiwa kutunza SIRI kuhusu kumbukumbu zote za maisha ya mwanachama binafsi, isipokuwa masuala ya utoaji na ukusanyaji wa mikopo ambayo kamati ya mikopo inaweza kuchukua hatua zozote za lazima dhidi ya wakopaji wasiokuwa waaminifu kwa maana ya kuwashirikisha wadhamini wao.

3. Vitabu vya hesabu na kumbukumbu nyingine za chama hiki zinaweza kuchunguzwa wakati wowote na kamati ya usimamizi ya chama hiki.

4. Kila mwisho wa mwaka wa fedha kiasi cha faida halisi kilichopatikana kinaweza kutolewa na Mkutano Mkuu kama tuzo kwa Meneja na wasaidizi wake kwa kufanya kazi kwa juhudi.

5. Mgogoro au malalamiko yoyote kuhusu masharti au huduma za chama hiki kati ya wanachama kwa wanachama, wanachama na watendaji, wanachama na wajumbe wa Bodi, wanachama na maafisa Ushirika, watendaji na wajumbe wa bodi, Bodi, watendaji na maafisa ushirika au wanachama wa zamani na wanachama wapya au watu wanaodai kupitia chama, yatapelekwa kwa Mrajis msadizi wa Vyama vya Ushirika mkoa na TUME ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

6. Chama kinaweza kufutwa katika daftari la Vyama vya Ushirika kwa amri ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika chini ya kifungu cha 100 cha sheria za vyama vya ushirika Na.6 ya mwaka 2013.

7. Mkaguzi aliyepitishwa na chama chini ya usimamizi wa TUME kuwa anakagua hesabu za chama ni COASCO ambaye hufanya ukaguzi wake akishirikiana na Kamati ya Usimamizi ya Chama kwa maana ya kupitia taarifa za ukaguzi wa kamati hiyo pamoja na taarifa ya ukaguzi ya Maafisa Ushirika.

Masharti haya yameandaliwa na Bodi ya chama chini ya usimamizi wa MRAJISI MSAIDIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA Mkoa kwa marejeo ya Sheria Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015.

WAJUMBE WA BODI YA CHAMA.

	JINA	SAINI:
1.	IGNATIUS NG'WANGA	
2.	PAUL MWAMBO	
3.	EZEKIEL J. SHOLLA	
4.	Thamary Mlewa	
5.	LISTER MALEGANA	
6.	George Nathan Malima	
7.	Specioza S. Kapela	
8.	.....	

TAREHE 29/04/2020 MUHURI WA CHAMA

NAKALA; 1. MRAJISI MSAIDIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA MKOA.
2. AFISA USHIRIKA JIJI.
3. WANACHAMA WOTE.

Registered this 07 day of May 2020
Asst. Registrar of Cooperative Societies

Certified as True Copy of the Original
Godfrey S.J. Wasonga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 07/05/2020